

# Mkate Wa Uzima Kutoka Mbinguni

Adrian Ebens
Carlos A. Hernández

# Mkate wa Uzima kutoka Mbinguni

Carlos A. Hernández na Adrian Ebens

Kimechapishwa na

MARANATHA MEDIA

maranathamedia.com

Kulisha watu elfu tano kunatupa mfano bora wa jinsi maisha ya Kristo yanatoa uhai. Muujiza huu ulitendeka muda mfupi kabla ya pasaka kuanza.

> Yohana 6:4,5 Pasaka ya Wayahudi ilikuwa imekaribia. Yesu alipotazama na kuuona ule umati mkubwa wa watu ukimjia, akamwambia Filipo, Tutanunua wapi mikate ili watu hawa wale?

Sikukuu ya mikate isiyotiwa chachu ikiwa imekaribia kutendeka, Yesu alikuwa na hamu ya kuwasaidia watu wake kugundua tena uwakilishi wa kiroho wa mkate katika uchumi wa Wayahudi? Anachukua mikate mitano na samaki wawili na kisha anaiongeza kuwa sherehe ya kulisha watu waume 5000 pamoja na wanawake na watoto. Watu walishangazwa walipoona miujiza na wakaanza kumtafuta Yesu. La kuhuzunisha, hawakuwa wakitafuta mkate wa kiroho ila mkate wa kimwili tu.

> Yohana 6:26 Yesu akawajibu, Amin, amin nawaambia, ninyi hamnitafuti kwa kuwa mliona ishara na miujiza, bali kwa sababu mlikula ile mikate mkashiba.

Hali hii inampa Yesu fursa ya kuwafunza watu mfano muhimu wa mkate na jinsi unamwangazia kama mpaji.

> Yohana 6:27 Msishughulikie chakula kiharibikacho, bali chakula kidumucho hata uzima wa milele, ambacho Mwana wa Adamu atawapa. Yeye ndiye ambaye Mungu Baba amemtia muhuri.

Yesu anawahimiza watu watazame zaidi ya kutafuta chakula cha mwili tu lakini badala yake chakula cha kiroho ambacho hutoa uzima wa milele. Chakula cha kiroho kinaweza toka tu kwa Kristo Yesu Bwana wetu. Watu kwa uhalisia walimuuliza Yesu jinsi wanaweza pata hiki. Jibu lake linashangaza:

> Yohana 6:28-29 Ndipo wakamwuliza, Tufanye nini ili tupate kuitenda kazi ya Mungu? (29)Yesu akawajibu, Kazi ya Mungu ndiyo hii: Mwaminini Yeye aliyetumwa Naye.

Kazi ambayo waliitiwa ilikuwa tu kumwamini Kristo kama Mwana wa Mungu aliye hai, Masihi aliye tumwa na Mungu kwa wokovu. Imani tu kwa Masihi waliyeahidiwa ingeruhusu Roho wa Yesu kuwajaza na kuwatia nguvu za

kuweka msingi imara kwa kushikilia uzima wa milele. Watu hawakuridhishwa na jibu hili. Walitaka ushahidi unaoonekana wa madai haya na kwa hivyo wakampa Yesu changamoto:

> Yohana 6:30-31 Hivyo wakamwuliza, Utafanya ishara gani ya mwujiza, ili tuione tukuamini? Utafanya jambo gani? (31) Baba zetu walikula mana jangwani, kama ilivyoandikwa, Aliwapa mikate kutoka mbinguni ili wale.

Roho mtamu wa kuburudisha wa Yesu akitenda kazi nafsini hawezi kuonekana. Huingia katika moyo wa yule ambaye ana imani kwa neno la Mungu kumhusu Masihi. Watu walitaka ishara inayoonekana na kisha wakarejerea kwa mfano wa mana ambayo ilitoka mbinguni kule jangwani. Kwa mara nyingine tena Kristo anawaelekeza katika uhalisia wa kiroho unaozunguka muujiza wa mana.

> Yohana 6:32-33 Yesu akawaambia, Amin, amin, nawaambia, si Musa aliyewapa mikate kutoka mbinguni, bali Baba Yangu ndiye anawapa mkate wa kweli kutoka mbinguni. (33) Kwa maana mkate wa Mungu ni yule ashukaye kutoka mbinguni na kuupa ulimwengu uzima.

Yesu anafafanua kina cha ukweli wa mfumo wa Uungu. Mkate wa kweli usioonekana ambao ulikuwa ukishuka kutoka juu ulikuwa ukidhihirishwa kupitia kwa mana. Kama wangebaini mfano huu ungewaelekeza kwa Kristo na wangetambua sababu tu ya mana hii kuanguka katika jangwa ni kuwa Kristo alikuwa akitoa nguvu za uzima wake ili kuwapa wao.

Yesu anarudia funzo hili kwa utaratibu kupitia aya zingine za sura ya sita. Zingatia kwa makini maneno haya:

> Yohana 6:48-51 Mimi ni mkate wa uzima. (49) Baba zenu walikula mana jangwani, lakini wakafa. (50) Lakini hapa kuna mkate utokao mbinguni, ambao mtu ye yote akiula, hatakufa. (51) Mimi ni mkate wa uzima ule uliotoka mbinguni. Mtu ye yote akiula mkate huu, ataishi milele. Mkate huu ni mwili wangu, ambao nitautoa kwa ajili ya uzima wa ulimwengu.’’

Uzima wote hutoka kwa Kristo na sasa Yesu anadhihirisha jinsi uzima huu huja kwetu.

> Yohana 6:51 … Mkate huu ni mwili wangu, ambao nitautoa kwa ajili ya uzima wa ulimwengu.

Yesu anafafanua hili zaidi:

> Yohana 6:53-55 Hivyo Yesu akawaambia, "Amin, amin, nawaambia, msipoula mwili wa Mwana wa Adamu na kuinywa damu Yake, hamna uzima ndani yenu. (54) Mtu ye yote aulaye mwili wangu na kunywa damu yangu, anao uzima wa milele. Nami nitamfufua siku ya mwisho. (55) Kwa maana mwili wangu ni chakula cha kweli na damu yangu ni kinywaji cha kweli.

Njia pekee ambayo Yesu anaweza tupa uzima huu ni kwa yeye kuteseka na kufa. Jaribu kuelewa uhusiano kati ya Kristo na uumbaji wake katika nukuu zifuatazo:

> Bwana wetu amesema, "Msipoula mwili wa Mwana wa Adamu na kuinywa damu Yake, hamna uzima ndani yenu…. Kwa maana mwili wangu ni chakula cha kweli na damu yangu ni kinywaji cha kweli." Yohana 6:53-55. **Hili ni kweli kwa hali yetu halisi. Kwa kifo cha Yesu tunawiwa na uzima wa sasa. Chakula tunachokula kimenunuliwa kwa mwili wake uliovunjwa. Na maji tunayokunywa, hutokana na damu yake iliyomwagika. Hakuna mtakatifu mmoja au mwenye dhambi alaye chakula chake Cha kila siku bila kuboreshwa na mwili na damu ya Kristo. Msalaba wa Kalwari umepigwa chapa juu ya kila kipande cha mkate; na nuru yake huonekana katika kila chemchemi ya maji.** Haya yote Kristo ametufunza kwa kuteua nembo ya sadaka yake kuu. Nuru inayong'aa kutoka katika Huduma ya meza ya Bwana huvitakasa vitu vyote vya maisha yetu ya kila siku. Mkusanyiko wa jamaa huwa sawa na meza ya Bwana na kila mlo Ushirika mtakatifu (sacrament). Tumaini la Vizazi Vyote, 660.3.

> "Yeye sio Mwanzilishi wa vyote tu bali ni uzima wa kila kitu kinachoishi. Ni uzima wake tunaopokea katika miale ya jua, kwa usafi, hewa tamu, na katika chakula ambacho huijenga miili yetu na kudumisha nguvu zetu." Education, 198.

Uzima wote ambao tunauona unadumu katika Maisha ya milele ya Kristo. Chakula chote tunachokula huja kwetu kupitia kukombolewa kwa damu. Nishati katika jua, mvua na ardhi ambayo inakuza mbegu za mazao yetu hutolewa na nguvu za Kristo kupitia kwa msalaba wake. Hili hutwelekeza kwa ukweli muhimu sana.

Chakula tunachokula hakina uzima wa kutuweka hai. Lakini chakula tunachokula ni njia ya nguvu za Kristo kuja kwetu. Nguvu hizi huwezeshwa kuja kupitia kwa chakula kwa sababu ya kafara kubwa ya Kristo msalabani. Hivo basi tunapozingatia mkate ambao tunaula, mkate huu halisi sio ambao unatuweka hai. Ila ni mkate wa kweli kutoka mbinguni ambao ni Kristo hutupa uhai.

> Juu ya vitu vyote vilivyoumbwa kunaonekana atathari ya Mungu. Maumbile yanamshuhudia Mungu. Mawazo ya kushukiwa, yakiletwa katika kukutana na miujiza na maajabu ya ulimwengu, hayawezi ila tu kutambua kazi ya uwezo mkubwa. Sio kwa nguvu zake mwenyewe ardhi inatoa neema yake, na mwaka baada ya mwingine unaendeleza mzunguko wake wa jua. Mkono usioonekana huongoza sayari katika mzunguko wake wa mbingu. Uzima wa ajabu uko kati maumbile – uzima ambao hudumisha vitu visivyohesabika kote ulimwenguni, uzima katika chembe ya wadudu ambao huelea katika upepo mwanana wa kiangazi, mabawa hayo ambayo husaidia kuruka kwa ndege na kulisha kunguru wachanga wanaolia, ambao hufanya mmea kuchipua ua na ua kuwa tunda.
>
> Nguvu hiyo hiyo ambayo hudumisha maumbile, pia inatenda kwa mwanadamu. Sheria kuu sawa na zile ambazo zinaongoza nyota na chembechembe zinatawala maisha ya mwanadamu. Sheria zinazotawala utenda kazi wa moyo, ukisawazisha mkondo wa mtiririko wa uzima mwilini, ni sheria za Akili yenye nguvu ambayo inamamlaka ya nafsi. Kwake yeye uzima wote hutoka. Ni kwa uiano naye tu ndiyo tunaweza pata ukweli wa nyanja ya tendo lake. Education 99.

Kuweka hili wazi, Kristo sio mkate; wala hayuko ndani ya mkate. Mkate ni njia ya uzima wake kutolewa kwetu. Kristo ni chemchemi, na mkate ni njia. Hivi viwili ni tofauti, ila kimoja kinapokelewa kupitia kwa kingine. Roho ya Unabii inaweka tofauti hii wazi kabisa kama ifuatavyo:

> Kazi ya mikono ya Mungu katika maumbile sio Mungu mwenyewe katika muambile. Vitu hivi vya maumbile ni dhihirisho la tabia ya Mungu; kupitia kwavyo tunaweza fahamu upendo wake, uwezo wake, na utukufu wake, lakini tusiyachukulie maumbile kama Mungu. Ujuzi wa kisanii wa mwanadamu hutengeneza kazi nzuri, vitu ambavyo hupendeza macho na vitu hivi hutupa kitu kuhusiana na wazo la msanii; lakini vitu vilivyoundwa sio mtu huyo. Sio kazi, bali mfanyakazi, ambaye anahesabiwa kustahili heshima. Hivyo, maumbile yakiwa ni udhihirisho wa wazo la Mungu, sio maumbile bali Mungu wa maumbile ambaye anafaa kutukuzwa. Testimonies Volume 8, 263

Watu ambao Yesu alikuwa akizungumzia waliona tu mkate halisi na wala hawangetafuta zaidi ili kuona nguvu za Kristo ambazo zinatolewa kupitia kwa mkate. Kwa maarifa haya mlo wote utasababisha mioyo yetu kujawa na upendo kwa Kristo, kwa upendo wake mkuu katika kutupa uzima kupitia kwa makala ya chakula ambayo tunaweza shiriki. Kama hatutambui ukweli huu basi chakula cha ulimwenguni ambacho tunakula hakiweza tuweka hai milele. Hili kwa uwazi linathibitisha kuwa chakula hakina uwezo wa kutupa uzima. Kinaweza tu kuwa gari au njia ya kutupa uzima.

Funzo ambalo Yesu alifundisha katika kuwalisha 5000 lilikuwa la kusaidia mawazo ya Israeli wakiwa katika kushiriki sikukuu ya mikate isiyotiwa chachu. Kila kipande cha mkate katika uchumi wa Wayahudi kilikuwa cha kufundisha funzo hili muhimu la uzima unaopatikana katika Kristo pekee.

Ukweli huu unazidisha maana ya sadaka ya nyama na vinywaji ambayo ilitolewa katika sadaka ya kila siku na pia katika Sabato, mwezi mpya na siku za sikukuu. Tunasisitiza hoja kuwa kila pumzi ambayo wanadamu wanapumua na kila sehemu ya chakula ambacho watu hula ni njia kwa uzima wa Kristo. Ni uweza wa Kristo ambao hupokelewa kupitia kwa mambo haya. Hii imekuwaa ndio hali tangia kuwekwa msingi kwa ulimwengu huu. Tunaona katika mfumo wa sadaka jinsi ukweli ungeelezewa na kueleweka.

> Hesabu 28:2 Waagize hao wana wa Israeli, uwaambie, Matoleo yangu, chakula changu cha sadaka zangu zisongezwazo kwa moto, za harufu ya kupendeza kwangu mimi, mtaangalia kuzisongeza kwangu wakati wake upasao.

Mkate unaorejelewa hapa ni sadaka ya nyama ambayo ilikuwa ikichanganywa kwa unga na mafuta na kisha kuokwa kwenye madhabahu pamoja na mnyama aliyetolewa kafara. Sasa tunagundua sadaka ya kafara ya kila siku.

> Hesabu 28:3-6 Nawe utawaambia, Hii ndiyo sadaka isongezwayo kwa moto mtakayomsongezea Bwana; wana-kondoo waume wa mwaka wa kwanza wakamilifu, wawili kila siku, wawe sadaka ya kuteketezwa ya siku zote. (4) Mwana-kondoo mmoja utamsongeza asubuhi, na mwana-kondoo wa pili utamsongeza jioni; (5) pamoja na sehemu ya kumi ya efa ya unga mwembamba kuwa sadaka ya unga, uliochanganywa na robo ya hini ya mafuta ya kupondwa. (6) Ni sadaka ya kuteketezwa ya siku zote, iliyoamriwa huko katika mlima wa Sinai iwe harufu ya kupendeza, sadaka ya kusongezwa kwa Bwana kwa moto.

Kila siku asubuhi na jioni mwana-kondoo alikuwa akitolewa. Pamoja na mwana-kondoo huyu sehemu ya kumi ya unga wa efa na robo ya hini ya mafuta zilitolewa. Vyanzo vingine vinasema kuwa efa moja ni kama lita 35[1] na vingine vinasema ni kama lita 22.[2] Urari huu ndio hoja yetu muhimu ya maelezo hivyo basi tutatumia kipimo cha lita 22 katika kijitabu hiki. Lita hupima ujazo ilihali kilo hupima uzito. Kilo 1 ya unga halisi ni kama lita 1.83. Hini ni kama galloni ambayo ni lita 3.6.[3] Hivyo basi kwa kila sadaka ya kila siku kulitolewa kilo 2.2 za unga zikichanganywa na mililita 900 au robo ya mafuta. Tukiweka hili katika jedwali tunapata yafuatayo:

---

[1] http://www.dictionary.com/browse/ephah ;
http://www.thefreedictionary.com/ephah

[2] http://www.convert-me.com/en/convert/history_volume/bibephah.html
http://bibleresources.americanbible.org/resource/weights-and-measures-in-ancient-israel
https://en.wikipedia.org/wiki/Ephah

[3] http://bibleresources.americanbible.org/resource/weights-and-measures-in-ancient-israel

| Sadaka | Wanyama | Jumla ya unga wa Sadaka | Jumla ya mafuta ya Sadaka |
|---|---|---|---|
| Kila siku | Wana-kondoo 2 – 1 asubuhi na 1 jioni<br><br>jumla = wana-kondoo 2 | Kilo 2.2 unga x 2 wa asubuhi na jioni.<br><br>Jumla = Kilo 4.4 | Lita 0.9 x 2 ya asubuhi na jioni.<br><br>Jumla = lita 1.8 |

Mkono mmoja wa unga na mafuta ukichanganywa pamoja uliteketezwa katika madhabahu kwa sadaka pamoja na mafuta ya ubani kiasi kisha mabaki ya unga na mafuta yalipeanwa kwa makuhani.

> Walawi 2:1-3 Na mtu atakapomtolea Bwana matoleo ya sadaka ya unga, matoleo yake yatakuwa ya unga mwembamba; naye ataumiminia mafuta, na kutia na ubani juu yake; (2) kisha atauleta kwa wana wa Haruni, hao makuhani; naye atatwaa konzi moja katika huo unga mwembamba, na katika mafuta yake, na huo ubani wote; kisha kuhani atauteketeza kuwa ndio ukumbusho wake juu ya madhabahu, ni kafara ya kusongezwa kwa njia ya moto, ya harufu ya kupendeza kwa Bwana; (3) na huo uliosalia wa ile sadaka ya unga utakuwa ni wa Haruni na wanawe; ni kitu kitakatifu sana katika sadaka zilizosongezwa kwa Bwana kwa njia ya moto.

> Walawi 10:12-14 Kisha Musa akanena na Haruni, na Eleazari, na Ithamari, hao wanawe waliobaki, Twaeni hiyo sadaka ya unga iliyosalia katika kafara za Bwana zilizotolewa kwa moto, mkaile pasipo kutiwa chachu, pale karibu na madhabahu; kwa kuwa ni takatifu sana; (13) nanyi mtaila katika mahali patakatifu, kwa sababu ni haki yako, na haki ya wanao, katika hizo kafara zisongezwazo kwa Bwana kwa moto; kwani ni hivyo nilivyoagizwa. (14) Na kidari cha kutikiswa, na mguu wa kuinuliwa, mtavila katika mahali palipo safi; wewe, na wanao, na binti zako pamoja nawe; kwa maana vimetolewa kuwa ni haki yako, na haki ya wanao, katika zile kafara za sadaka za amani za wana wa Israeli.

Kristo alijidhihirisha yeye mwenyewe kama mkate wa uzima katika Yohana 6. Mkate usiotiwa chachu ulioandaliwa kwa unga na mafuta ulikuwa njia

iliyoangazia uzima uliopo katika Kristo. Mkate huu wa kweli ulishuka vipi kutoka mbinguni? Ulikuja kupitia kwa kafara ya uzima wa Kristo kwa ulimwengu. Hili lilitambuliwa vipi katika sadaka ya kila siku? Ilikuwa kupitia kwa kafara ya mwana-kondoo. Hivyo kafara ya mwana-kondoo ilikuwa utambulisho wa uzima wa Kristo unaotolewa ili kupokea Roho Mtakatifu. Ukweli huu ulionyeshwa katika mchanganyiko wa unga na mafuta ukiunganishwa kama mkate wa kuliwa na makuhani. Nao kwa wakati huo wangekuwa watoaji wa neema kwa Waisraeli wengine. Leo, wale ambao wanaamini katika Kristo ni sehemu ya ukuhani wa kifalme na wote wanaweza shiriki katika mkate huu wa uzima.

> 1 Petro 2:9 Lakini ninyi ni taifa teule, ukuhani wa kifalme, taifa takatifu la Mungu, mlioitwa ili kutangaza sifa Zake Yeye aliyewaita kutoka gizani mkaingie katika nuru Yake ya ajabu.

Je, hili linaongeza maana mpya kwa sala ya Bwana? Angazia hoja hii:

> Mathayo 6:11 Utupatie leo mkate wetu wa kila siku.

Kila asubuhi na kila jioni katika sadaka ya kila siku mkate ambao ulitolewa uliwakilisha mkate wa kweli ambao ulitoka mbinguni na uwezo wa Kristo kufanya hili uliwasilishwa katika kifo cha mwana-kondoo kila siku. Tunapoamba "Utupatie leo mkate wetu wa kila siku" tunawaza kuhusu mkate wa kweli wa Mungu ambao hushuka kutoka mbinguni au tu mkate halisi?

Uwezo wa Waisraeli wa kuishi, kupumua, kula na kunywa ulikuwa tu kwa sababu ya mkate wa kweli ambao ulitoka mbinguni. Kinachovutia zaidi ni kutambua kinachotendeka kwa sadaka ya siku ya Sabato.

> Hesabu 28:9-10 Tena katika siku ya Sabato watasongezwa wana-kondoo wawili, waume wa mwaka wa kwanza, wakamilifu, pamoja na sehemu ya kumi mbili za efa za unga mwembamba kuwa sadaka ya unga, uliochanganywa na mafuta, pamoja na sadaka yake ya kinywaji; (10) hii ndiyo sadaka ya kuteketezwa ya kila Sabato, zaidi ya hiyo sadaka ya kuteketezwa ya siku zote, pamoja na sadaka yake ya kinywaji.

Katika siku ya Sabato sadaka na kafara ya nyama iliongezwa maradufu:

| Sadaka | Wanyama | Jumla ya Unga | Jumla ya Mafuta |
|---|---|---|---|
| Kila siku –mwana-kondoo 1 asubuhi na 1 jioni. | Wana-kondoo 2<br><br>Jumla =wana-kondoo 2 | Kilo 2.2  x 2<br><br>Jumla = kilo 4.4 | Lita 0.9  x 2<br><br>Jumla = lita 1.8 |
| Sabato | Wana-kondoo 2 na wana-kondoo 2 wa kila siku.<br>Jumla =  wana-kondoo4 | Kilo 4.4 na kilo 4.4 sadaka ya kila siku.<br>Jumla = kilo 8.8 | Lita 1.8 na lita 1.8 sadaka ya kila siku.<br>Jumla = lita 3.6 |

Swali muhimu ambalo lazima liulizwe ni mbona kila kitu kinakuwa maradufu katika siku ya Sabato? Tena tunakumbushwa kuwa mkate na kila tone la mafuta ni njia ya uzima wa Kristo kuja kwetu. Nyama na vinywaji halisi na zilizoonekana zilikuwa zikiangazia nyama na vinywaji vya kiroho ambavyo vilitoka mbinguni kuja ulimwenguni kupitia kwa Kristo. Paulo anaelezea kwa njia hii:

> 1 Wakorintho 10:1-4 Zaidi ya hayo ndugu zangu, sitaki mkose kufahamu ukweli huu kwamba baba zetu walikuwa wote chini ya wingu na kwamba wote walipita katikati ya bahari. (2) Wote wakabatizwa kuwa wa Mose ndani ya lile wingu na ndani ya ile bahari. (3) Wote walikula chakula kile cha roho, (4) na wote wakanywa kile kinywaji cha roho, kwa maana walikunywa kutoka katika ule mwamba wa roho uliofuatana nao, ule mwamba ulikuwa Kristo.

Musa alipougonga mwamba na maji yakatoka kwake, hawakuwa wanapokea maji halisi tu, walikuwa pia wakishiriki katika uzima wa Kristo. Maji yenyewe hayangewaweka hai. Ilikuwa Roho wa Yesu ndiye aliwaweka hai. Hii ndio sababu wote walikunywa kinywaji hiki cha kiroho sio tu mwenye haki. Tena tunakumbushwa:

> Mathayo 5:45 ili mpate kuwa watoto wa Baba yenu aliye mbinguni. Kwa maana Yeye huwaangazia jua lake watu waovu na watu wema, naye huwanyeshea mvua wenye haki na wasio haki.

> Yohana 1:9 Nuru halisi, imwangaziayo kila mtu ilikuwa inakuja ulimwenguni.

Uzima wa Kristo unatolewa kwa watu wote kupitia kwa njia ambayo ameteua. Wale ambao hawatafuti zaidi ya chakula na kinywaji halisi hatimaye watakufa kwa kukataa kutambua chemchemi ya uzima. Hii ndio maana Yesu alisema kwa hadhira yake:

> Yohana 6:32-33 Yesu akawaambia, Amin, amin, nawaambia, si Musa aliyewapa mikate kutoka mbinguni, bali Baba Yangu ndiye anawapa mkate wa kweli kutoka mbinguni. (33) Kwa maana mkate wa Mungu ni yule ashukaye kutoka mbinguni na kuupa ulimwengu uzima.

Mana ambayo ilianguka kule jangwani haikutoka kwa Musa. Na wala sio mana yenyewe iliyowaweka hai. Ni uzima wa Kristo kupitia kwa mana ambao uliwaweka hai. Huu ndio mkate wa kweli kutoka mbinguni. Waisraeli wote walikula na kunywa kutoka kwa nyama na vinywaji vya kiroho lakini karibu wote walifia jangwani kwa sababu hawakutafuta zaidi ya chakula na maji ya kimwili. Tukiwa na mawazo haya akilini wacha turejee kwenye swali la unga, mafuta na sadaka zaidi siku ya Sabato.

Bibilia inatwambia kuwa Mungu aliitakasa Sabato. Akaifanya takatifu. A.T Jones anaelezea hili wazi anaposema:

> Sasa kitu kingine: Nani alikuwa wakala wa kweli katika uumbaji? [Kusanyiko: "Kristo."] Ni nani huyo ambaye alipumzika? [Kusanyiko: "Kristo."] Ni nani aliburudishwa? [Kusanyiko: "Kristo."] Ni nani aliibariki? [Kusanyiko: "Kristo."] Ni uwepo wa nani uliifanya takatifu? [Kusanyiko: "Kristo."] Ni uwepo wa nani ulioko katika siku hii? [Kusanyiko: "Kristo."] Kisha mtu ambaye uwepo wa Yesu Kristo haumtakasi, na haumfanyi takatifu na haumbariki na kwa ambaye hauleti pumziko, mbona, hawezi itunza Sabato. **Hauoni kwamba, ni kuwa na Kristo katika mtu tu ndio Sabato inawezatunzwa; kwa sababu Sabato huleta na inauwepo wa Kristo ndani yake**. A.T Jones, GCB 1893, Sermon 20.

Sasa zingatia hoja hii muhimu ambayo A.T. Jones anasema:

> Je, mtu, kwa wakati huo, katika bustani ya Edeni, akiwa jinsi Mungu alivyomuumba, alijua yote kumhusu Mungu ambayo angejua daima? [Kusanyiko: "Hapana."] **Basi kila siku ya Sabato ilipofika, ingemletea ufahamu zaidi na uwepo wa Mungu. Lakini huyu ni nani? [Kusanyiko: "Kristo."] Ufahamu zaidi na uwepo wa Kristo mwenyewe.** Basi kama angesalia mwaminifu, bado angekua katika ufahamu wa Mungu, mwenyewe, katika uzoefu wake, akikua zaidi na zaidi katika yote ambayo ni hali ya Mungu. A.T Jones, GCB 1893, Sermon 20.

Kwa hivyo Sabato inafanya maradufu uwepo wa Kristo kwetu. Je, hiki ndicho kinaonyeshwa katika tofauti kati ya sadaka ya kila siku na sadaka ya Sabato? Kuna sehemu maradufu ya sadaka, unga na mafuta. Je, kiwango kikubwa cha sadaka hakitwambii kuwa kuna karama kubwa ya roho ambayo inatolewa kwetu katika siku hii? Hii hapa ahadi ya Bwana

> Isaya 58:13-14 Kama ukigeuza mguu wako usihalifu sabato, usifanye anasa yako siku ya utakatifu wangu; ukiita sabato siku ya furaha, na siku takatifu ya Bwana yenye heshima; ukiitukuza, kwa kutokuzifanya njia zako mwenyewe, wala kuyatafuta yakupendezayo, wala kusema maneno yako mwenyewe; (14) ndipo utakapojifurahisha katika Bwana; nami nitakupandisha mahali pa nchi palipoinuka; nitakulisha urithi wa Yakobo baba yako; kwa maana kinywa cha Bwana kimenena hayo.

Tukijua kwamba kuna mibaraka zaidi katika siku ya Sabato na zaidi kuwa mibaraka hii ni Roho wa Kristo, Sabato inatufunza kuwa Mungu ana wakati ambao analeta uwepo wa Yesu karibu zaidi nasi kuliko wakati mwingine. Hili linazaliwa na kifungu hiki katika Isaya.

> Isaya 48:18 Laiti ungalisikiliza amri zangu! Ndipo amani yako ingalikuwa kama mto wa maji, na haki yako kama mawimbi ya bahari:

Kristo ni haki yetu. Isaya anatwambia kuwa haki hii ni kama mawimbi ya bahari. Mawimbi ya bahari huenda katika mawimbi binafsi ambayo hupanda na kushuka kwenye ufuo wa bahari. Na pia wakati wa mchana kuna tufani mbili kuu. Kisha wakati wa mwezi mpya na mwezi kamili kuna tufani falme. Hivi vitu vyote vinatuzungumzia juu ya kupwa na kutiririka kwa Roho wa haki wa Kristo ambaye huja kwa wana wa Adamu.

Ufunguo wa kuifahamu Sabato ni kujua kwamba kuna wakati wa kipekee ambao Kristo huja karibu nasi zaidi. Ukweli huu unaonekana katika tofauti kati ya sadaka ya kila siku na sadaka ya Sabato. Pindi tu tutakaposhika kanuni hii basi tutakuwa tayari kuona kitu cha kupendeza zaidi.

> Walawi 26:2-4 Zishikeni Sabato zangu, na kupastahi patakatifu pangu; mimi ndimi Bwana. (3) Kama mkienda katika amri zangu, na kuyashika maagizo yangu, na kuyafanya; (4) ndipo nitazinyesha mvua zenu kwa nyakati zake, na nchi itazaa maongeo yake, na miti ya mashambani itazaa matunda yake.

Kuikumbuka sabato ni kukumbuka kuwa Bwana ana majira ya kipekee ya kufanya upya kile ameteua. Kupastahi Patakatifu ni kukumbuka gharama kubwa kwa Baba yetu na Bwana Yesu katika kutupa karama hii. Tunapoikumbuka Sabato na kupastahi Patakatifu basi mvua itatunyeshea kwa wakati wake na mashamba yatanawili.

Tunakumbuka kuwa mvua na chakula ni njia ya uzima wa Kristo kupeanwa kwetu. Jinsi neema hii inavyokuwa kubwa ndivyo ushahidi kuwa uzima wa Kristo unapitishwa kupitia kwa njia hizi unavyoonekana. Tunapoifungua mioyo yetu kwa shukrani kwa sababu ya karama hii basi tunakuwa katika sehemu ya kuweza kupokea zaidi. Tunapomtukuza Bwana katika Sabato kwa sababu ya Roho maradufu basi mvua hii haitanyesha karibu nasi bali itanyesha juu yetu na itanawili katika neema. Kama wanajua au hawajui kila mtu duniani anafaidika kutokana na kafara ya kila siku ya Yesu. Kama tulivyogundua awali Mungu huinyesha mvua kwa wenye haki na wasio haki. Wote hupokea utoaji wa kila siku lakini wale tu ambao huitikia wito wa Mungu kupitia kwa sheria zake watapokea mibaraka zaidi ambayo inapatikana katika Sabato na teuzi zingine za kipekee.

Kitu cha kupendeza kuhusiana na ukweli huu wa Sabato hii ni kuwa mto ambao hutiririka kutoka Patakatifu unaongezeka kwa kina kadri unavyotiririka.

> Ezekieli 47:1-4 Baadaye akanileta tena mpaka lango la nyumba; na tazama, maji yalitoka chini ya kizingiti cha nyumba, kwa njia ya

> mashariki, maana upande wa mbele wa nyumba ulielekea upande wa mashariki; nayo maji yakashuka toka chini ya upande wa kuume wa nyumba, upande wa kusini wa madhabahu. (2) Ndipo akanileta nje kwa njia ya lango upande wa kaskazini, akanizungusha kwa njia ya nje mpaka lango la nje, kwa njia yake iliyoelekea mashariki; na tazama, maji yalitoka upande wa kuume. (3) Na alipotoka mtu yule, mwenye uzi wa kupimia mkononi mwake, kwenda masharikini, akapima dhiraa elfu, akanivusha maji yale; maji yakafika mpaka viweko vya miguu. (4) Kisha akapima dhiraa elfu, akanivusha maji yale, maji yakafika mpaka magoti. Kisha akapima dhiraa elfu, akanivusha, maji yakafika mpaka viuno.

Tunaona kuwa kama jinsi maji yalivyotoka hekaluni, yangeongezeka kwa kina. Kidokezo cha mahali maji haya yanatiririka ili kuongezeka kwa kina kinapatikana katika sura ya awali.

> Ezekieli 46:3-8, 11 Watu wa nchi nao wataabudu mbele ya mlango wa lile lango mbele za Bwana, siku za sabato, na siku za mwezi mpya. (4) Nayo sadaka ya kuteketezwa, ambayo mkuu atamtolea Bwana siku ya sabato, itakuwa wana-kondoo sita wakamilifu, na kondoo mume mkamilifu. (5) Na sadaka ya unga itakuwa efa moja kwa kondoo mume, na sadaka ya unga kwa wale wana-kondoo, kiasi awezacho kutoa, na hini moja ya mafuta kwa efa moja. (6) Na siku ya mwezi mpya itakuwa ni ng'ombe mume mchanga mkamilifu; na wana-kondoo sita, na kondoo mume; nao watakuwa wakamilifu. (7) Naye atatengeneza sadaka ya unga, efa moja kwa ng'ombe mume, na efa moja kwa kondoo mume, na kwa wale wana-kondoo, kwa kiasi awezacho kutoa, na hini moja ya mafuta kwa efa moja. (8) Naye mkuu atakapoingia, ataingia kwa njia ya ukumbi wa lango lile, naye atatoka kwa njia iyo hiyo… Na katika sikukuu hizo, na sikukuu nyingine zilizoamriwa, sadaka ya unga itakuwa efa moja kwa ng'ombe mmoja, na efa moja kwa kondoo mume mmoja, na kwa wale wana-kondoo kiasi awezacho kutoa, na hini moja ya mafuta kwa efa moja.

Kiwango cha sadaka kiliongezeka walivyotoka katika kila siku kwa sabato kwa mwezi mpya na kisha kwa sikukuu. Orodha ya sadaka katika Ezekieli 46 ni tofauti kidogo na ile ambayo inaorodheshwa katika vitabu vya Musa. Tutaonyesha mpangilio kutoka kwa Musa hapa. Sijajumuisha sadaka ya vinywaji lakini inafuata mpangilio sawa.

| Sadaka | Wanyama | Jumla ya Unga wa Sadaka | Jumla ya Mafuta ya Sadaka |
|---|---|---|---|
| Kila siku.Hes 28:3-6<br>Mwana-kondoo 1 asubuhi na 1 jioni | Wana-kondoo 2<br>**Jumla =wana-kondoo 2** | unga kilo2.2 x 2<br>**Jumla = kilo 4.4** | Lita 0.9 x 2<br>**Jumla = lita 1.8** |
| Sabato. Hes 28:9,10 | Wana-kondoo 2 pamoja na 2<br>**Jumla = wana-kondoo 2** | 4.8kilo pamoja na 4.8kilo kutoka sadaka ya kila siku.<br>**Jumla = kilo 8.8** | 1.8 lita pamoja na 1.8 lita<br>**Jumla = lita 3.6** |
| Mwezi mpya. Hes 28:11-14 | Dume wachanga 2,<br>kondoo 1<br>wana- kondoo 7 pamoja na sadaka ya kila siku.<br>Mwana-mbuzi 1 wa kafara ya dhambi. | 6.6x2 = 13.2kilo<br>4.4x1= 4.4 kilo<br>(2.2x7)+(2.2x2) =19.8kilo<br>**Jumla = kilo 37.4** | 2.7x2 dume<br>1.8x1 kondoo<br>0.9x7 wana-kondoo<br>0.9x2 wana-kondoo wa kila siku<br>**Jumla = lita 15.3** |
| Pasaka. Kut 12:21 | Mwana-kondoo wa Pasaka | Mkate usiotiwa chachu | Mboga kali |
| Mikate isiyotiwa chachu kwa siku 7. Hes 28:17-25<br>7 x mwezi mpya | Dume 14<br>Kondoo 7<br>Wana-kondoo 49 + 14 wa kila siku + 2 Sabato<br>Mwana-mbuzi 7 | Kilo 37.4 x siku 7 + kilo 4.4 za Sabato<br>**Jumla = kilo 266.2**<br>(mara 60.5 ya kila siku) | 15.3 lita x 7 + 1.8 lita za Sabato ya kila wiki<br>**Jumla = lita 108.9** |
| Sikukuu za wiki | Dume wachanga 2, kondoo 1 na wana-kondoo 7. Pamoja na wana-kondoo 2 wa sadaka ya kila siku.<br>Mwana-mbuzi 1 | 3/10 ya dume kwa siku<br>2/10 ya kondoo kwa siku<br>1/10 ya wana-kondoo kwa siku | 2.7x2 dume<br>1.8x1 kondoo<br>0.9x7 wana-kondoo<br>0.9x2 wana-kondoo kila siku |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | wa sadaka ya dhambi | Hesabu = (6.6x2)+(4.4x1)+ (2.2x7)+(2.2x2)<br>**Jumla = kilo 37.4** | **Jumla = lita 15.3** |
| Sikukuu ya Tarumbeta. Hes 29:1-6 Ilifanyika katika mwezi mpya. Hivyo sadaka ilijumuisha sadaka ya kila siku na ya mwezi mpya na ya tarumbeta. | Dume 1+2<br>Kondoo 1+1<br>Wana-kondoo 7+7+2<br>Wana-mbuzi 2 | 6.6x3 = kilo 19.8<br>4.4+4.4 = 8.8 kilo<br>16x2.2 = 35.2 kilo<br>**Jumla = kilo 63.8** | 2.7x3 = lita 8.1<br>1.8 x2 = lita 3.6<br>0.9 x16= lita 14.4<br>**Jumla = lita 26.1** |
| Siku ya Upatanisho. Hes 29:7-11 | Dume 1<br>Kondoo 1<br>Wana-kondoo 7 lambs + 2 wa kila siku<br>Mwana-mbuzi 1 | 6.6kilo<br>4.4kilo<br>19.8kilo<br>**Jumla = kilo 30.8** | 2.7x1 = lita 5.4<br>1.8x1 = lita 1.8<br>0.9x7 + 0.9x2 = lita 8.1<br>**Jumla = lita 15.3** |
| Sikukuu ya Vibanda. Hes 29:12-40<br>Siku 1 = dume wachanga 13, Siku 2 = dume 12, Hadi 7 = dume 7.<br>Kila siku = kondoo 2 na wana-kondooo 14 | Dume 70<br>Kondoo 14<br>Wana-kondoo 98 + 14 kila siku + 2 wa Sabato<br>Wana-mbuzi 7 wa kafara ya dhambi. | 462 kilo<br>61.6 kilo<br>250.8 kilo<br>**Jumla = kilo 774.4** | 2.7x70 = lita 189<br>1.8x14 = lita 25.2<br>0.9x 114 = lita 102.6<br>**Jumla = lita 316.8** |

Ili kutupa mtazamo wa jinsi mto huongezeka kwa kina kadri unavyotiririka kutoka kwa karama ya Roho ya kila siku hadi kwa sikukuu ya vibanda tutatoa viwango vya unga na mafuta. Hatutaorodhesha sadaka za zote za wiki na Mwezi Mpya ila tu kupanga kuanzia kwa kila siku hadi sikukuu ya mwisho kwenye kalenda.

| Sadaka | Unga | Mafuta | Ezekieli 47:1-7 Mto |
|---|---|---|---|
| Kila siku | Kilo 4.4 | Lita 1.8 | Maji kutoka Patakatifu |
| Sabato | Kilo 8.8 | Lita 3.6 | Katika dhiraa 1000 yanafika kwenye viweko vya miguu |
| Mwezi Mpya | Kilo 37.4 | Lita 15.3 | Katika dhiraa 2000 yanafika kwenye magoti it reached the knees |
| Mkate Usiotiwa chachu | Kilo 266.2 (30 x Sab. sadaka) | Lita 108.9 | Katika dhiraa 3000 yanafika kwenye viuno |
| Sikukuu ya Mwezi wa saba | Kilo 869 (~100x Sab. sadaka) | Lita 359.2 | Katika dhiraa 4000 yanafika hadi kichwani |

Kinachovutia zaidi kuhusu mto huu ni kuwa kila mahali ambapo ulifika ulileta uzima na uponyaji.

> Ezekieli 47:9 Tena itakuwa, kila kiumbe hai kisongamanacho, kila mahali itakapofika mito hiyo, kitaishi; kutakuwapo wingi mkubwa wa samaki, kwa sababu maji haya yamefika huko maana maji yale yataponyeka, na kila kitu kitaishi po pote utakapofikilia mto huo.

Sabato inatupa kanuni ya ongezeko la kiwango cha uwepo wa Kristo. Tukiendelea katika mtindo huu pamoja na teuzi zingine tunaona kuwa maji yanazidi kuongezeka kwa kina hata zaidi. Kama vile Sabato ni kama kuwa na maji kwa viweko vya miguu, hivyo makuhani wa Israeli walikuwa wakiweka miguu yao kwenye maji kabla ya mto wote kufunguka kwao, Yoshua 3:13. Kama unaikumbatia Sabato kwa imani basi mengine yote ya mto yatafunguka kwako ili kupita. Unga na mafuta yaliyochanganywa pamoja ili kuandaa mkate ambao hutoka mbinguni. Kama tukiona zaidi ya vitu halisi kwa mkate

wa kweli kama unavyopatikana kwa Kristo basi tumegundua mto wa kuongezeka kwa kina ambao hutoka kwenye kiti cha enzi cha Mungu.

Tambua tena kuwa Ezekieli aliporudi tena kwenye ukingo wa mto katika alama ya dhiraa elfu nne, kulikuwa na miti kila mahali.

> Ezekieli 47:7 Basi nikiisha kurudi, tazama, kando ya ukingo wa mto ilikuwapo miti mingi sana, upande huu na upande huu.

Mto ulitoa maji ya kutosha ili kwamba miti ikue kikamilifu na kuzaa mingine thelathini, mingine sitini na mingine mara mia moja ya ile iliyopandwa. (Marko 4:20).

Hapa kuna siri ya mto wa uzima. Tunapofuata nyakati na misimu ya kunawili kutoka kwa Bwana; kama tukitembea katika sheria ya Bwana na kukumbuka amri zake na hukumu basi tunafungua mioyo yetu kwa imani kuwa miti iliyopandwa kandokando ya vijito vya maji.

> Zaburi 1:2-3 Bali sheria ya Bwana ndiyo impendezayo, Na sheria yake huitafakari mchana na usiku. (3) Naye atakuwa kama mti uliopandwa Kandokando ya vijito vya maji, Uzaao matunda yake kwa majira yake, Wala jani lake halinyauki; Na kila alitendalo litafanikiwa.

Katika hali hii ya mawazo inasema kuwa matawi yetu hayawezi kunyauka kumaanisha kwamba dhambi haiwezi kututawala. Uzima wa Kristo ambao ni mkate kutoka mbinguni utapokelewa kikamilifu na njaa yetu na kiu ya haki itatoshelezwa. Je, hii ndio sababu Roho ya Unabii ilikuwa na hamu kuhimiza watu kuwa na ibada ya asubuhi na jioni?

> Saa zilizoteuliwa kwa sadaka ya asubuhi na jioni [354] zilichukuliwa kuwa takatifu, na zilitunzwa kama saa zilizowekwa za ibada katika taifa lote la Wayahudi. Na kisha baadaye Wayahudi walipotapakaa kama wafungwa katika inchi za mbali, bado katika saa hiyo teule waligeuza nyuso zao kuelekea Yerusalemu na kutoa maombi yao kwa Mungu wa Israeli. Katika desturi hii Wakristo wana mfano wa maombi ya asubuhi na jioni. Ingawa Mungu anakemea mzunguko wa sherehe tu, bila roho wa ibada, huangalia kwa furaha kubwa wale ambao wanampenda, wakiinama asubuhi na jioni ili kutafuta msamaha wa dhambi ambazo

> wamezitenda na kuwasilisha ombi la mibaraka wanayohitaji. Patriarchs and Prophets 353,354.

Kama kuna mkate wa uzima ambao unakuja kwetu asubuhi na jioni basi sio jambo la busara kupumzika na kukusanya mkate huu kwa nafsi zetu?

Tunaona jinsi Roho ya Unabii inaunganisha sadaka ya asubuhi na jioni ya Israeli na ibada yetu ya asubuhi na jioni. Licha ya ukweli kuwa kuna wakati wa kipekee wa kuabudu kila siku inaonyesha sana kuwa mkate wa uzima bado unatushukia asubuhi na jioni kwanzia mwanzo wa kumwabudu Mungu wa kweli ulimwenguni.

Kama tukikusanyika kila asubuhi na jioni na pia tukusanyike kila Sabato kwa mibaraka maradufu basi mbona tusizidi ridhaa 3000 zaidi katika chemchemi ya Sabato na tupokee maji ya uzima ya kutosha kuzuia nafsi zetu kukauka na kuruhusu dhambi kutawala katika maisha yetu. Tunapewa onyo hili:

> Ezekieli 47:11 Bali mahali penye matope, na maziwa yake, hayataponywa; yataachwa yawe ya chumvi.

Maziwa na matope ni mahali ambapo wakati mmoja yalipokea maji ya kutiririka lakini sasa hapako kwenye maji ya kutiririka tena. Hawa ni wale wamepokea nuru ya Baba na Mwana lakini wamekataa kuiendeleza kwa kilio cha usiku wa manane. Wao watashuhudia maziwa na matope yakiachwa kuwa chumvi ambayo haiwezi kuza chochote. Kuja katika mtiririko wa uzima na upokee mkate wa uzima kupitia kwa teuzi za Baba na utabarikiwa.

Kafara na sadaka zote katika sheria ya Musa zilielekeza kwa karama ya Roho ambayo inapatikana kupitia kujitoa kwa Kristo. Kafara hii haikuashiria maisha ya baadaye tu bali pia iliashiria mto wa uzima ambao kwa wakati huo ulitiririka kupitia kwa misimu ya kunawili kutoka kwa Baba yetu na Bwana Yesu.

Je, unatamani tu kupokea maji ambayo yanafika kwenye viweko vya miguu tu? Badala yake haungetaka maji ya kutosha ambayo hukufika juu ya kichwa na kukuruhusu kuwa mti kandokando ya mto? Inatendeka vipi? Tafakari mchana na usiku kuhusu sheria ya Mungu ambayo itakupa wakati wa misimu

ya kunawili. Kisha katika msimu huu utapokea hekima na utambuzi wa jinsi ya kusoma Bibilia na kuiweka katika maisha yako.

Kuna wengi siku ya leo ambao hawafunzi kuwa msalaba wa Kristo uko karibu nao. Kwa kusisitiza kuwa mfumo wa kutoa kafara wa Wayahudi uliashiria tu mateso ya Kristo miaka 1500 katika maisha ya baadaye kutoka kwa Musa kisha hitimisho ambayo inatolewa ni kuwa msalaba wa Kristo sasa umepita miaka 2000. Kujikana nafsi kwake kwa sasa na kuteseka kukubwa katika kuubeba msalaba leo kunapunguzwa na hata kupuuzwa. Hili tu ni kama vile Shetani anataka liwe. Gundua kile A.T Jones anasema kuhusu hili.

> Tatizo kubwa na Wayahudi tangia mwanzo hadi mwisho lilikuwa na kuwa na Bwana mbali zaidi kwamba hata vitu ambavyo alikuwa amewapa kusimamia ukaribu wake mkamilifu vilichukuliwa kama ishara yake ya kuwa mbali. **Sadaka, kafara, vibanda, hekalu, huduma yake, vitu hivyo vyote vilitumiwa na walimu wa Wayahudi na kundi kubwa la watu katika njia ambayo kile ambacho huduma hii yote ilimaanisha kwao kuwa ilimwashiria Kristo mbali kule**. Ilifahamika kuwa vitu hivi vilimaanisha Masihi, lakini ilikuwa Masihi aliye mbali kabisa. Na lazima [476] wangejifanya wema ili kumleta karibu, na vitu hivi vilitazamwa kama kuwa na wema ndani yao wenyewe na kwa hivyo kuweza kutoa matendo mema.
>
> **Sina uhakika kama Waadventista wa Sabato wako na wazo zaidi ya vitu hivyo vya awali, kuwa vilimsimamia Kristo aliye mbali. Lakini sisemi kuwa Waadventista wa Sabato wanafikiria kuwa Kristo sasa yuko mbali. Lakini nahofia kuwa bado hawajaondoka kwenye wazo hilo, wanapotazama patakatifu na huduma yake, sadaka na kafara, ambayo ilikusudiwa kuwafunza kuhusu umbali wa Kristo kule. Hivyo inasemekana kuwa vitu hivi vyote vilimwashiria Kristo. Vitu vyote vilimwashiria Kristo, huo ndio ukweli. Lakini ni Kristo karibu sio mbali. Mungu alikusudia kuwa vitu hivi vingemwashiria Kristo akiishi mioyoni mwao, sio miaka 1800 iliyopita, sio mbali zaidi kama mbingu ilivyo kwa nchi, bali ikimwashiria Kristo katika maisha yao ya siku baada ya siku. Tutakaposhika wazo hilo kwanza na kisha kusoma patakatifu, kafara, sadaka, kwa kifupi, injili kama ilivyo katika Walawi –basi tutaona kuwa Kristo anaishi, mkombozi**

**aliyopo kwao siku baada ya siku na pia tutaona ndivyo alivyo kwetu leo pia.**

**Kuna injili, kuna uzoefu wa Kikristo, kwetu leo katika Walawi, katika Kumbukumbu, Katika Mwanzo, katika Kutoka, na katika Bibilia nzima. Lakini tunaposoma mafungu haya na kusema kuwa sadaka na kafara hizo zote zilimwashiria Kristo aliye mbali zaidi kutoka kwa Wayahudi na kutarajia kuwa Wayahudi wangetazama kupitia kwa huduma hii ya njia ya mbali kwa Kristo kuja wakati mmoja—tunaposoma maandiko hayo na kuyatazama kwa njia hiyo, basi tunasoma maandiko hayo kwa juu kama Wayahudi walivyofanya na tunasimama kwa uwazi walipo kuwa kwa wakati huo katika maandiko hayo.**

Hilo hatutatenda daima. Hapana. Hatupaswi kutazama patakatifu kwa samani yake na vitu ambavyo Mungu aliviweka, kwa uwepo wa Mungu hapo ndani, na mawazo kwamba aliwaonyesha kuwa walikuwa wajifunze kwayo kwamba Mungu aliishi tu katika patakatifu mbinguni. Tunapoitazama kwa jinsi hiyo, basi tuko tayari kufikiria kuwa hilo ni kuhusu kuwa karibu kama alivyo karibu kwetu, kwa sababu hiyo na karibu kama tulivyosikia akija kwao. Kwa kuwa kama tukitazama kwa niaba yao kwa njia hiyo, basi kama tungekuwa pahali pao, tungelitazamaje kwa niaba yetu sisi wenyewe? Kwa njia sawa, na hii inaonyesha kuwa kama tungekuwa hapo tungekuwa hasa kama walivyokuwa.

Tabia hii, iko pia nasi, ya kusoma patakatifu na huduma zake na kukaa kwa Mungu katika patakatifu na kifungu, "Nao na wanifanyie patakatifu; ili nipate kukaa kati yao," na kusema, Ndio, Mungu alikaa nao katika patakatifu na hiyo iliashiria patakatifu pa mbinguni na wakati waja ambao Mungu atakaa na watu wake tena, kwa maana anasema juu ya nchi mpya, "Tazama, makao ya Mungu ni pamoja na wanadamu, naye atakaa pamoja nao. Yeye atakuwa Mungu wao nao watakuwa watu wake." Basi inchi mpya itakapokuja Mungu ataishi na watu wake tena. Lakini Mungu yuko wapi sasa? Hilo ndilo tunalotaka kujua. Kinachojalisha kwangu ni kwamba atakaa na watu wake katika nchi mpya? Nini kinajalisha kwa haya yote, kama hakai na mimi sasa? Kwa kuwa kama hawezi kaa na mimi sasa, ni hakika kwamba daima hawezi kaa na mimi katika nchi mpya wala pengine popote, kwa maana hana fursa. Kile ambacho nahitaji kujua na kila nafsi inahitaji kujua ni, je,

> anakaa na mimi sasa? Kama tukimweka mbali kule katika siku za Wayahudi na kisha kumweka mbali kabisa, hilo linafanya nini kwetu? Hilo linamtoa vipi kwa wanadamu sasa? Katika njia hiyo, anakaa aje nasi sasa? Hilo ndilo tunahitaji kujifunza kila wakati.
>
> **Sasa, unaweza ona kuwa kuna mpango mkubwa zaidi katika mfumo wa utaratibu wa sherehe kuliko tu kitu kidogo cha muda ambacho kiliwasumbua Wayahudi kwa muda na kisha kutoweka. Kwa kuwa hali ya mwanadamu bado ni, na daima inasumbuliwa nayo bila shaka kama shetani anavyoishi, kama hakika kama uadui ulivyo katika moyo wa mwanadamu. Mawazo hayo ambayo sio kwa sheria ya Mungu, wala kwa kweli yanaweza kuwa—tu kama bila shaka kama ilivyo katika ulimwengu, kama tu dunia iishivyo italaaniwa kwa utaratibu wa sherehe. Na kama kuna chochote cha namna hiyo moyoni mwangu, nitakuwa katika hatari ya kulaaniwa na sherehe.**

Nitaingia katika mistari ya mawazo ya Jones na kusema kuwa lazima isemwe kwamba wale ambao wanafundisha kwamba Wayahudi walihusishwa katika mzunguko tu wa haki na utaratibu wa sherehe kwa wokovu ambao ulikuwa miaka 1500 mbele yao wanafundisha Mungu wa utaratibu wa sherehe. Kama Mungu alikuwa tu Mungu wa utaratibu wa sherehe kabla ya msalaba basi sifa hii inasalia katika tabia yake na kwa kushikilia hili tunabadilishwa kuwa watu wa kufuata utaratibu wa sherehe. Tahadhari na uwe na utambuzi wa wale ambao wanaunga mkono utaratibu wa sherehe hata kama wanapanga dhidi yake. Wacha tuendelee na kile A.T. Jones anasema:

> Kile ambacho tunapaswa kufanya ni kutafuta ukombozi huu katika Yesu Kristo, Ushindi wa hakika na kukwezwa katika mkono wa kuume wa Baba wa mbinguni, katika yeye, kwamba uadui huo utaondolewa ndani yetu katika yeye. Kisha tutakuwa huru kwa utaratibu wa sherehe; Kisha tutakuwa huru na utamaduni na sheria za wanadamu, na watu kujitengenezea dhamiri zao kwetu. Wanadamu wanasema, “Lazima ufanye hili au hauwezi okolewa. Lazima ufanye lile au hautaokolewa." La, la, Mwamini Yesu Kristo au hautaokolewa. Kuwa na imani ya kweli katika Yesu Kristo na umeokolewa.
>
> Ni vita sawa na vile ambavyo vilipiganwa katika siku na kazi ya Paulo. Alikuwa akimhubiri Yesu Kristo pekee kwa wokovu. Lakini Mafarisayo

fulani “ambao waliamini” walimfuata kila mahali, wakisema "Oh, ndio, ni vyema zaidi kuamini katika Yesu Kristo, lakini kuna [477] kitu kingine. Lazima utahiriwe na utunze sheria za Musa ama ukose kuokolewa." Mashindano hayo yaliendelea kwa miaka na dhidi ya yote Paulo alipigana wakati wote. Hangelegeza hata kidogo kwa wakati wowote. "Mkitahiriwa, Kristo hatawafaidi neno." "Ninyi mtakao kuhesabiwa haki kwa sheria; mmeanguka na kutoka katika hali ya neema." Hakuna, hakuna chochote ila Kristo na imani katika yeye! Vyema, waliipeleka katika baraza mwishowe, na hapo Roho wa Mungu akaamua kuwa Kristo na wala sio utaratibu wa sherehe ndio njia ya wokovu. Hicho ndicho kisa kizima. Moja lilikuwa jaribio la kufunga utaratibu wa sherehe juu ya Ukristo au badala ya pahali pa ukristo; na nyingine ilikuwa kanuni ya kudumu ya Yesu Kristo kwa imani ya kudumu, ikiendesha uzima na moyo wa wale wanaoamini ndani yake.

Kuna tofauti kubwa kati ya utaratibu wa sherehe na kanuni. Yesu Kristo anataka tumtafute kikamilifu na kibinafsi ili kwamba kanuni za kudumu za ukweli wa Mungu, kama zilivyo katika Yesu Kristo, zitakuwa mwongozo wetu na kwamba hizo kanuni za kudumu zinazong’aa katika maisha ya mwanadamu kwa utukufu wa Yesu Kristo zitakuwa mwongozo wetu kila mahali, na tutajua cha kufanya kwa wakati. Basi hatuhitaji maazimio au kiapo chochote kutulazimisha kufanya hili, lile, au lingine. Hiyo ndio tofauti kati ya utaratibu wa sherehe na kanuni ya kudumu ya uwepo wa Kristo katika moyo. Moja ni desturi na huduma ya nje, bila Kristo; na nyingine ni yote katika Kristo na Kristo wote na katika yote.

Wacha tuangalie tena vitu ambavyo Wayahudi walikuwa wakifanya kule nyuma katika huduma ya hekaluni, sadaka na kafara ili kwamba uone hili ila kikamilifu zaidi. Ninajua na pia nawe unajua kwamba patakatifu, hekalu, ilikuwa inawakilisha patakatifu pa mbinguni, kwamba kafara ilikuwa inawakilisha kafara ya Yesu Kristo na ukuhani na huduma yake ilikuwa inawakilisha ukuhani wa Kristo. Kupitia kwa vitu hivi Mungu angewafunza na kutufunza sisi kujihusu yeye mwenyewe kama anavyodhihirishwa katika Kristo. Mwanzo kulikuwa na patakatifu na kulikuwa na hekalu ambalo lilinjengwa pahali pa patakatifu. Kulikuwa na hekalu juu ya Mlima Sayuni katika Yerusalemu. Na kutoka kwa hilo, Mungu aliwafundisha kuwa kule ndiko hekalu la kweli juu ya Mlima Sayuni katika Yerusalemu ya mbinguni. Mungu alikaa katika hekalu hili juu ya Mlima Sayuni katika

Yerusalemu, katika Palestina, na kwa hilo aliwaonyesha kwamba alikaa kule katika hekalu la mbinguni juu ya Mlima Sayuni, katika Yerusalemu ya mbinguni.

Na alisema pia—na hili lilikuwa kweli katika pahali pote na pande zote mbili--" Maana yeye aliye juu, aliyetukuka, akaaye milele; ambaye jina lake ni Mtakatifu; asema hivi; Nakaa mimi mahali palipoinuka, palipo patakatifu." Pengine popote? "Tena pamoja na yeye aliye na roho iliyotubu na kunyenyekea." Lini? Tunasoma mbali na kule. Ni lini alikaa "pamoja na yeye aliye na roho iliyotubu na kunyenyekea," na vile vile "mahali palipoinuka, palipo patakatifu?" je, alifanya hili miaka mia saba kabla ya Kristo, Isaya aliponena? Ndio. Lakini Bwana alianza tu wakati huo kukaa pamoja na yeye aliye na roho iliyotubu na kunyenyekea, na vile vile mahali palipoinuka, palipo patakatifu juu ya Mlima Sayuni? La.

Miaka elfu moja kabla ya Kristo, Daudi alipozungumza, alifanya hivyo wakati huo? Ndio. Lakini alikuwa ameanza wakati huo? La. Daima, milele, anakaa pahali pote pa wili--pamoja na yeye aliye na roho iliyotubu na kunyenyekea na vile vile palipoinuka.

Vyema, basi, Mungu hukuwafunza, katika hekalu hilo la duniani, sio tu jinsi alivyokaa katika nchi ya mbinguni, bali jinsi alikaa katika hekalu la moyo pia? Kwa hakika zaidi, kulikuwa na Mlima Sayuni duniani mbele ya macho yao, kiwakilishi cha Sayuni ya mbinguni, ambayo Mungu alikuwa nayo mbele ya macho yao ya imani. Juu ya Mlima Sayuni, mahali palipoinuka, palipo patakatifu katika Yerusalemu ya duniani, kulikuwa na hekalu na Mungu akikaa katika hekalu. Na katika hili Mungu angeonyesha kuwa hakukaa tu pale bali pia katika hakalu la moyo, patakatifu pa nafsi, pa aliye na roho iliyotubu na kunyenyekea. Na katika kuweka hekalu lake miongoni mwa watu waovu na kukaa ndani yake yeye mwenyewe, alikuwa akionyesha pia jinsi atakaa yeye mwenyewe katika mwili wa Kristo, miongoni mwa watu waovu na katika miili yenye dhambi.

Pia kulikuwako na ukuhani wa hekalu la duniani juu ya Mlima Sayuni katika Yerusalemu. Kulikuwa na ukuhani wa patakatifu kule Shilohi katika jangwa. Hilo, ni kweli, liliwakilisha ukuhani wa Kristo, lakini je hilo liliwakilisha ukuhani wa Kristo kabla ya A. D. 1? Tunaweza sema kuwa hilo liliwakilisha ukuhani wa Kristo ambao ulikuwa mbali kabisa?

> La, ukuhani katika Yerusalemu, katika patakatifu pa jangwani, uliwakilisha ukuhani ambao tayari ulikuwapo kwa mfano wa Melkisedeki? Kutakuwa na kuhani hata milele, kwa mfano wa Melkisedeki? La, la. "Ndiwe kuhani hata milele, kwa mfano wa Melkisedeki." Melkisedeki hakuwa kuhani katika siku za Ibrahimu? Na ukuhani wa Kristo sio wa milele, kwa mfano wa Melkisedeki?
>
> Hauoni, basi, kuwa mfumo huu wote wa huduma uliotolewa kwa Israeli ulikuwa kuwafundisha uwepo wa Kristo wakati huo na kwa hivyo ukombozi wa sasa [478] wa nafsi zao na sio ukombozi wa nafsi zao miaka elfu moja mia nane au elfu mbili au elfu nne ijayo? Hakika, hakika, ndivyo ilivyo. March 5, 1895 ATJ, GCB 477.7

Rafiki zangu natarajia na kuomba kuwa mtatambua mto huu wa thamani wa uzima ambao unapatikana katika mkate wa uzima kutoka mbinguni na unadhihirishwa katika sadaka ya nyama, ya unga na mafuta. Unga huu uliochanganywa na mafuta uliashiria Mkate wa kweli wa Mungu ambao ulikuwepo kwao wakati huo na hapo kwa wokovu. Kwa njia sawa tunaweza sogea kila siku na kila Sabato na kila mwezi mpya na kila sikukuu tukiwa na utambuzi wa kina wa mto wa uzima na karama ya Roho. Sabato kweli ni njia ya mhuri wa Mungu. Mara tunapoingia katika kanuni ya Sabato tunakiri kwamba Mungu hutuma Roho wake kwa msimu wa kipekee. Tunapokesha na kuomba kwa Baba yetu kutualika katika msimu wake alioteua basi wakati huo tutapokea mkate wa uzima zaidi kabisa kuliko kiwango cha kila siku kinachopeanwa kwa watu wote.

Kama uko tayari kuja kwa Mungu kila asubuhi na kuamini kuwa Mkate wa Uzima kwa kweli unakuja katika ibada ya asubuhi kama inavyoonyeshwa katika sadaka ya nyama ya kafara ya asubuhi basi ni mbaraka wa aina gani utafurahia katika imani hii. Jambo sawa linatendeka tena katika sadaka ya jioni. Ni hisia gani ya hamu, hili linaleta tunapokuja katika imani kupokea mkate wa uzima ambao hushuka kutoka mbinguni. Je, unaamini kuwa kuna sehemu maradufu ambayo inakuja katika Sabato kama inavyoonyeshwa katika Injili ya Agano la Kale? Je, unaamini kuwa mwezi mpya unakupa mibaraka mara nane kutoka kwa karama ya kila siku ya mkate kutoka mbinguni? Je, ni u mbali gani ambao ungependa kufika katika mto huu wa

uzima? Je, Una njaa na kiu ya haki ya Kristo? Shikilia nyakati za Mungu za kunawilisha na ufungue moyo wako kwa imani kwa mkate wa kweli ambao hushuka kutoka mbinguni na hautaaibishwa.

> Yohana 6:52-64 Ndipo Wayahudi wakaanza kuhojiana vikali wao kwa wao wakisema, Mtu huyu awezaje kutupatia mwili wake tuule? (53) Hivyo Yesu akawaambia, Amin, amin, nawaambia, msipoula mwili wa Mwana wa Adamu na kuinywa damu Yake, hamna uzima ndani yenu. (54) Mtu ye yote aulaye mwili wangu na kunywa damu yangu, anao uzima wa milele. Nami nitamfufua siku ya mwisho. (55) Kwa maana mwili wangu ni chakula cha kweli na damu yangu ni kinywaji cha kweli. (56) Ye yote alaye mwili wangu na kunywa damu yangu, atakaa ndani yangu nami nitakaa ndani yake. (57) Kama vile Baba aliye hai alivyonituma Mimi, na kama nami ninavyoishi kwa sababu ya Baba, hivyo anilaye mimi ataishi kwa sababu yangu. (58) Huu ndio mkate ushukao kutoka mbinguni, si kama ule mkate baba zenu waliokula nao wakafa. Lakini yeye aulaye mkate huu ataishi milele. (59) Yesu alisema maneno haya alipokuwa akifundisha katika sinagogi huko Kapernaumu. (60) Wengi wa wafuasi Wake waliposikia jambo hili wakasema, Mafundisho haya ni magumu. Ni nani awezaye kuyapokea? (61) Yesu alipojua kwamba wafuasi Wake wananung'unika kuhusu mafundisho Yake, akawaambia, Je, jambo hili limewaudhi? (62) Ingekuwaje basi kama mngemwona Mwana wa Adamu akipaa kwenda Zake huko alipokuwa kwanza? (63) Roho ndiye atiaye uzima, mwili haufai kitu. Maneno haya niliyowaambia ni Roho tena ni uzima. (64) Lakini baadhi yenu hamwamini. Kwa maana Yesu alifahamu tangu mwanzo wale ambao hawangemwamini miongoni mwao na yule ambaye angemsaliti.

Basi ni leo. Umati mkubwa hauamini katika mto huu wa uzima wenye thamani. Baadhi yao hata wako kazini sasa kuharibu sifa za ndugu zao labda tu waipate nuru ya ukweli huu. Kwa kweli malighafi ya kijitabu hiki ni msemo mgumu kwa wengi. Je, hili linakukwasa pia?

> Yohana 6:65-67 Akaendelea kusema, Hii ndiyo sababu niliwaambia kwamba hakuna mtu awezaye kuja kwangu isipokuwa amejaliwa na Baba Yangu. (66) Tangu wakati huo wafuasi Wake wengi wakarejea nyuma wakaacha kumfuata. (67) Hivyo Yesu akawauliza wale wanafunzi Wake kumi na wawili, Je, ninyi pia mnataka kuondoka?

Ilikuwa kupitia kwa mafundisho kuhusu kanuni ya mkate wa uzima ambapo watu wengi walirejea nyuma kutoka kwa Yesu na wakaacha kumfuata. Lakini tunatiwa moyo kwa maneno ya wanafunzi:

> John 6:68-69 Simoni Petro akamjibu, Bwana, tuondoke twende kwa nani? Wewe unayo maneno ya uzima wa milele. (69) Tunaamini na kujua kuwa Wewe ndiwe Kristo Mwana wa Mungu aliye hai.

Wacha huu uwe ushuhuda wetu ili tuweze kuomba kwa furaha, “Utupe leo mkate wetu wa kila siku,” na tuamini kwamba utaongezeka kwa jinsi sawa Yesu aliongeza mikate na samaki na kuwalisha watu 5000 mda mchache kabla ya kumwagwa kwa Roho wakati wa sikukuu ya mikate isiyotiwa chachu.

Kabla tumalize funzo hili tunahitaji kuangazia swali la sadaka ya kinywanji ikiunganishwa na mkate na kafara na tuone kwa kina zaidi jinsi furaha ya Baba na Mwana inapeanwa kwetu kwa Roho wa neema.

> Hesabu 28:7 Na sadaka yake ya kinywaji itakuwa robo ya hini kwa mwana-kondoo mmoja; hiyo sadaka ya kinywaji, ya kileo, utammiminia Bwana katika mahali hapo patakatifu.

Katika fungu la 7 tunapata kirai *kileo* (*shakár-* Stong’s H7941). Baadhi ya fasiri wanairejelea kama *divai bora* badala ya *kileo*; hili linakubaliana na Walawi 2:11 ambayo inasema “Sadaka ya unga **iwayo yote** itakayosongezwa kwa Bwana **isitiwe chachu** kabisa; kwa kuwa hamtateketeza **chachu**, wala asali iwayo yote, kuwa ni sadaka ya kusongezwa kwa Bwana kwa njia ya moto.” (YLT). Kuwa sadaka hii ya kinywaji ilihusisha divai na wala sio kinywaji kingine chochote inaweza dhibitishwa na Hesabu 15:1-10 ambapo agizo la kutoa pamoja na sadaka ya wanyama wa sikukuu (pia inatajwa katika Hesabu 28) sadaka ya kinywaji cha *yayin* Strong’s H3196 ni wazi ni zao la mzabibu. Watafsiri wengi wanaiweka kama kileo, au kinywaji kilichochachishwa, lakini hili huleta upinzani katika maandiko yanayohusiana na Walawi 2:11. Baba hangeagiza sadaka ambayo inasimamia mbaraka anaotoa, kwa kitu anachokemea. Tukichunguza tafsiri za Kihispania za fungu hili, tunagundua kuwa karibu zote (isipokuwa za katoliki) zinaweka “divai bora”. *Reina-Valera Revisada* kuanzia 1909, 1960, 1994, 1995, 2000, 2004 zote zinaiweka “divai

bora”. Tafsiri ya *Sagradas Escrituras (1569)* pia inaiweka kama “divai bora”. *Biblia Latinoamericana 1995* iliitafsiri “divai nzuri”. Tafsiri ya *Jubilee Bible 2000* inasema:

> Na sadaka yake ya kinywaji itakuwa robo ya hini kwa mwana-kondoo mmoja; hiyo sadaka ya kinywaji, **divai bora**, utammiminia Bwana katika mahali hapo patakatifu.

Pia, ufafanuzi wa Bibilia wa S.D.A. unasema yafuatatayo (tafsiri kutoka Kihispania):

> “Wachambuzi wengi wanasisitiza kuwa katika hali hii *shekári* lazima irejelee divai nzuri na yenye cheo kikubwa. Wachambuzi wa kiyahudi, kwa kanuni moja, wanashikilia kuwa katika hali hii, kutokana na matumizi ya *shekári*, dhana ya divai iliyotiwa maji haipo, na kwa upande mwingine, wanapendelea wazo la divai safi iliyomamacitwa”.

Hili linatupa nafasi ya kuwaza kuwa divai bora inaweza maanisha haijatiwa maji, sharubati ya mzabibu. Pia iko katika mkataba na kubadilishwa kwa maji kuwa divai iliyofanywa na Yesu kwenye harusi ya Kana, wakati mkuu wa karamu alisema bwana harusi alihifadhi divai nzuri iwe ya mwisho. Dhana ya “divai nzuri”, “divai safi” au “divai safi iliyomamacitwa” inaingiana kikamilifu na lugha inayopatikana katika Tumaini la Vizazi vyote:

> “Kando ya mlango kulikuwako na mabalasi makubwa sita, Yesu aliwaambia watumishi wayajaze maji. Na likafanywa. Kisha wakati divai ilihitajika kutumika kwa wakati huo, alisema, “Choteni sasa maji hayo mkampelekee mkuu wa karamu,” badala ya kuwa maji tu, yakageuka kuwa divai tamu. Sio mkuu wa karamu wala wageni waliokuwa wamejua kuwa divai ilikuwa imeisha. Walipoionja hiyo iliyoletwa na watumishi, mkuu wa karamu akaona kuwa ni **tamu** kuliko yote aliyopata kunywa, na tofauti kabisa na ile walikunywa katika mwanzo wa sherehe. Akimgeukia bwana harusi, alisema, “Kila mtu hutanguliza kuleta divai nzuri, na watu wakisha shiba, huleta ile mbaya, lakini wewe umengoja na divai nzuri hadi sasa.” – {DA 148.2}

Zingatia uhusiano kati ya divai na mibaraka ambayo Mungu hutoa kupitia kwa Kristo.

“Kama jinsi watu hutanguliza kuleta divai nzuri, na kisha baadaye divai mbaya, ndivyo ulimwengu ulivyo na zawadi zake. Zawadi zinazotolewa na ulimwengu zinaweza pendeza macho na kuleta utamu, lakini zinathibitisha hazitoshelezi. Divai hugeuka chungu, shangwe hugeuka kuwa majonzi. Kilichoanzishwa kwa nyimbo na shangwe huishia katika uchungu na ghasia. **Lakini zawadi ya Yesu ni mpya daima. Karamu anayoandaa kwa nafsi zetu haikosi kututosheleza na kutupa furaha. Kila zawadi huzidisha uwezo wa mpokeaji kuthamini na kufurahia mibaraka ya Bwana.** Hutupa neema kwa neema. Hakuwezi kuwa na upungufu. Ukidumu katika yeye, ukweli kwamba unapokea zawadi nzuri leo ni hakikisho la zawadi bora kesho. Maneno ya Yesu kwa Nathanaeli yanaonyesha sheria ya Mungu ikikabiliana na wana wa imani. Kwa kila ufunuo mpya wa upendo wake, anatangaza kwa moyo wenye kupokea, “Unaamini kwa kuwa nilikuambia nilikuona ulipokuwa bado uko chini ya mtini? Basi utaona mambo makuu zaidi kuliko hilo.” Yohana 1:50. – {DA 148.3}

“**Divai iliyofanywa na Yesu karamuni**, na ile aliyowapa wanafunzi kama mfano wa damu yake mwenyewe, **ilikuwa sharubati kamili ya mzabibu**. Hii ndio nabii Isaya anarejelea anapozungumzia divai mpya “katika kichala,” na anasema, “Usikiharibu **kwa maana mna baraka ndani yake**.” Isaya 65:8. – {DA 149.3}

Kama diva hii nzuri na safi ni mfano wa mibaraka ya Kristo, basi sadaka ya kinywaji kutoka Hesabu 28:7 ambayo inapaswa kumaanisha mbaraka lazima iwe ya hali moja. Mtu anaweza leta sadaka kwa Mungu akitambua kwamba mwanzo ni yeye aliyempa. Mungu hakuwapa watu vinywaji viliyochachishwa na kutiwa sumu. Mungu alitoa furaha yake safi na isiyochanganywa katika Mwanawe.

Pia zingatia usawa wa neno *shekári* na kitenzi *shakári* ambalo kulingana na Strong’s H7937 linaweza maanisha kuwa na shukurani au kunywa kwa wingi. Tunaona basi kuwa sadaka ya divai ilikuwa ya divai mpya, na ilimaanisha baraka iliyotolewa na Mungu kwa watu wake.

Hesabu 28:7 inatupa kiwango cha divai kwa kila mwana-kondoo na Hesabu 28:14 inatupa kiwango cha divai kwa kila dume na kondoo na kurudia kiwango cha wana-kondoo.

> Hesabu 28:14 Tena sadaka zake za vinywaji zitakuwa nusu ya hini ya divai kwa ng'ombe, na sehemu ya tatu ya hini kwa kondoo mume, na robo ya hini kwa mwana-kondoo; hii ndiyo sadaka ya kuteketezwa ya kila mwezi katika miezi yote ya mwaka.

Hesabu ni kama ifuatavyo:

| Sadaka | Unga | Mafuta | Divai |
|---|---|---|---|
| Kila siku | Kilo 4.4 | Lita 1.8 | Lita 1.8 |
| Sabato | Kilo 8.8 | Lita 3.6 | Lita 3.6 |
| Mwezi Mpya | Kilo 37.4 | Lita 15.3 | Dume 2 = hini1; mwana-kondoo 1 = hini 1/3; wana-kondoo 7 = hini ¼ x 7.<br>**Jumla = lita 11.1** |
| Mkate usiotiwa Chachu | Kilo 266.2 (30 x sadaka ya Sabato ) | Lita 108.9 | **Lita 11.1 x 7 = lita 77.7** |
| Pentecosta | Kilo 37.4 | Lita 15.3 | Lita 12.9 |
| Sikukuu ya Mwezi wa Saba | Kilo 869 (~100x Sadaka ya Sabato) | Lita 359.2 | Tarumbeta = lita 22.2<br>Upatanisho = lita 11.1<br>Vibanda = lita 245.4 ltrs<br>**Jumla = lita 278.7** |

Unga uliotumiwa kutengeneza mkate, unawakilisha uzima ambao Mungu anatoa na kudumisha kupitia kwa Mwanawe katika ulimwengu wote; Mafuta, pia yanatumika kutengeneza mkate, lakini pia ni mfano wa roho anayetolewa kwa wana wa Mungu, lakini vipi kuhusu divai? Mara nyingi ni mfano wa damu ya Kristo, lakini katika muktadha wa sadaka haiwezi kuwa kwa sababu tayari kuna aina ya damu katika mwana-kondoo aliyechinjwa. Katika muktadha huu

sadaka ya divai inakuwa mfano wa kitu ambacho damu ya Kristo ilinunua kwa ajili yetu.

Mkate, unajumuisha unga na mafuta, na divai ni mfano wa mibaraka. Kwa mfano, wakati Abrahamu alirejea kutoka kumwokoa mpwa wake Loti, Melkizedeki alikuja kumlaki ili kumbariki na akaleta mkate na divai kwa Abrahamu.

> **Mwanzo 14:18,19** Na Melkizedeki mfalme wa Salemu akaleta **mkate** na **divai**, naye alikuwa kuhani wa Mungu Aliye juu sana. (19) Akambariki, akasema, Abramu na abarikiwe na Mungu Aliye juu sana, Muumba mbingu na nchi:

Kufuatia baraka hii Abrahamu alikuwa na hakikisho kuwa alihifadhiwa na Mungu, na hakuhitaji miungu ya wanadamu, na akakataa kuukubali utajiri wa ufalme wa Sodoma.

> Mwanzo 14:21-23 Mfalme wa Sodoma akamwambia Abramu, Nipe mimi hao watu, na hizo mali uchukue wewe. (22) Abramu akamwambia mfalme wa Sodoma, Nimeinua mkono wangu kwa Bwana, Mungu Aliye juu sana, Muumba mbingu na nchi, (23) ya kuwa sitatwaa uzi wala gidamu ya kiatu wala cho chote kilicho chako, usije ukasema, Nimemtajirisha Abramu:

Kitabu cha Yoeli kinatumia, unga, mafuta, na divai kama ishara za mibaraka ya Mungu.

> Yoeli 2:19 Bwana akajibu, akawaambia watu wake; Tazameni, nitawaletea nafaka, na divai, na mafuta, nanyi mtashiba kwa vitu hivyo; wala sitawafanya tena kuwa aibu kati ya mataifa:

Jina la nafaka ni *dagan* Strong's H1715 na humaanisha mbegu, mkate au ngano. Tukiwa na hili mawazoni wacha tuangazie Zaburi ifuatayo:

> Zaburi 104:1-15 Ee nafsi yangu, umhimidi Bwana. Wewe, Bwana, Mungu wangu, Umejifanya mkuu sana; Umejivika heshima na adhama. (2) Umejivika nuru kama vazi; Umezitandika mbingu kama pazia; (3) Na kuziweka nguzo za orofa zake majini. Huyafanya mawingu kuwa gari lake, Na kwenda juu ya mabawa ya upepo, (4) Huwafanya malaika

> zake kuwa pepo, Na watumishi wake kuwa moto wa miali. (5) Uliiweka nchi juu ya misingi yake, Isitikisike milele. (6) Uliifunika kwa vilindi kama kwa vazi, Maji yalikuwa yakisimama juu ya milima. (7) Kwa kukemea kwako yakakimbia, Kwa sauti ya radi yako yakaenda zake kasi, (8) Yakapanda milima, yakatelemka mabondeni, Mpaka mahali ulipoyatengenezea. (9) Umeweka mpaka yasiupite, Wala yasirudi kuifunikiza nchi. (10) Hupeleka chemchemi katika mabonde; Zapita kati ya milima; (11) Zamnywesha kila mnyama wa kondeni; Punda mwitu huzima kiu yao. (12) Kandokando hukaa ndege wa angani; Kati ya matawi hutoa sauti zao. (13) Huinywesha milima toka orofa zake; Nchi imeshiba mazao ya kazi zako. (14) Huyameesha majani kwa makundi, Na maboga kwa matumizi ya mwanadamu; Ili atoe chakula katika nchi, (15) Na **divai** imfurahishe mtu moyo wake. Aung'aze uso wake kwa mafuta, Na **mkate** umburudishe mtu moyo wake.

Kifungu hiki kinaelezea maana ya aina tatu ya sadaka ambazo zimetajwa katika Hesabu 28, na muktadha wa Zaburi ni Mungu kama mpaji na mhifadhi wa uzima. Tunaweza ona mkate kama ishara ya uzima wa Kristo ukitolewa kwa wanadamu huupa nguvu na kuudumisha moyo wa mwanadamu, mafuta kama ishara ya Roho wa Kristo huufanya uso wa mwanadamu kumeremeta, na divai kama ishara ya furaha ya Kristo huufanya moyo wa mwanadamu kufurahia.

Kuna mafungu mengi ambayo huwasilisha divai kama furaha na kupendezwa. Mojawapo ni mfano katika Waamuzi 9.

> Waamuzi 9:12, 13 Kisha miti ikauambia mzabibu, Njoo wewe, utawale juu yetu. Huo mzabibu nao ukaiambia, Je! Niiache **divai** yangu, ambayo **humfurahisha** Mungu na wanadamu, ili niende nikayonge-yonge juu ya miti?

Neno hapa la humfurahisha ni *samakj* Strong’s H8055 na ni neno sawa ambalo linatumika katika Zaburi 104:15. Katika Zaburi hii tunaona kuwa divai huifanya mioyo ya wanadamu kufurahia, na katika Waamuzi 9:13 humfurahisha Mungu na mwanadamu. Ni jinsi gani diavai inaweza mfurahisha Mungu? Ni nini ambacho tunajua kuhusu furaha na radhi ya Baba? Ambaye katika yeye ninapendezwa? Methali 8:30 inasema:

> Methali 8:30 Ndipo nilipokuwa pamoja naye, kama stadi wa kazi; Nikawa furaha yake kila siku; Nikifurahi daima mbele zake;

Na katika Mathayo 3:17 inasema:

> Matthew 3:17 Nayo sauti kutoka mbinguni ikasema, Huyu ni Mwanangu mpendwa, ambaye ninapendezwa sana naye.

Kristo, Mwana wa pekee wa Mungu, ndiye kupendezwa, furaha na radhi ya Baba. Kuna uhusiano mzuri wa furaha kati ya Kristo na Mungu Baba yake. Kristo anafurahia katika agape ya Baba inayoonekana kwa kumteua Mwanawe kama mrithi wa vitu vyote, na Baba anafurahishwa na anapendezwa vizuri katika Mwanawe, ambaye anathamini upendo wake wa kujikana nafsi, na anashiriki kila kitu alichorithi na ulimwengu. Kristo alipokea ili kutoa, na anashiriki na wanadamu kupendezwa na furaha ya uhusiano kati yao wote. Roho ya unabii inasema:

> "Na maneno yaliyonenwa kwa Yesu katika Yordani, "Huyu ni Mwanangu mpendwa, ambaye ninapendezwa sana naye," yanakumbatia ubinadamu. Mungu alizungumza kwa Yesu kama mwakilishi wetu. Na dhambi zetu zote na udhaifu, hatuwekwe kando kama wasiofaa. "Kwa hiyo tunamsifu Mungu kwa huruma zake kuu alizotumiminia kwa sababu sisi ni wa Mwanae Mpendwa." Waefeso 1:6. DA 113

> Methali 8:30 Ndipo nilipokuwa pamoja naye, kama stadi wa kazi; Nikawa furaha yake kila siku; **Nikifurahi daima mbele zake.**

Kristo anaeneza furaha yake kwa wanadamu. Kufurahia kwa Baba juu ya Mwanawe, na kufurahia. kwa Mwana sio tu mbele ya Baba, bali pia na wanadamu. Divai kama ishara ya furaha na kupendezwa, inamwasilisha Kristo kama furaha ya Mungu na wanadamu. Kristo ni furaha ya Mungu, na furaha ya kweli ya mwanadamu inaweza tu kuwa Mwana mpendwa wa Mungu.

Ishara nyingine ya Kristo ambayo huunganika na divai kama ishara ya furaha na kupendezwa ni mto wa uzima. Zaburi 46:4 inasema:

> Zaburi 46:4 Kuna mto, vijito vyake **vyaufurahisha** mji wa Mungu, Patakatifu pa maskani zake Aliye juu.

Neno hapa la furaha tena ni *samakj*, na tunaweza ona kuwa mto huu katika mji wa Mungu unafurahisha mji wote. Kulingana na Ufunuo 22 mto huu hutiririka kutoka kwa kiti cha enzi cha Mungu na Mwana-kondoo. Je, hii inaweza kuwa ishara ya furaha ya Baba katika Mwanawe ikishirikiwa na ulimwengu kupitia kwa Kristo, njia? Ninaamini hivyo. Kwangu mimi, kitu kizuri zaidi kuhusu hivi vyote ni kuwa divai ya Mbingu, furaha ya Mbingu na kupendezwa kumetolewa kwetu bure.

Wacha tutazame fungu lingine.

> Zaburi 36:7-9 Ee Mungu, jinsi zilivyo na thamani fadhili zako! Wanadamu huukimbilia uvuli wa mbawa zako. Watashibishwa kwa unono wa nyumba yako, **Nawe utawanywesha mto wa furaha zako**. Maana **kwako Wewe iko chemchemi ya uzima**, Katika nuru yako tutaona nuru.

Katika fungu la 9 tunaona kuwa chemchemi ya uzima inarejelewa kama kuwa na Mungu. Tunajua kuwa Bibilia inafundisha kuwa Baba ndiye chanzo kikuu cha kila kitu, hapa tunaona kitu au mtu aliye na Mungu akirejelewa kama chemchemi ya uzima. Katika Methali 8 tunamwona Kristo akiwa na Mungu, katika Yohana 1:1 kuwa neno alikuwako na Mungu, na katika Ufunuo tunamuona mwana-kondoo akiketi na Mungu katika kiti chake cha enzi. Hapa tunaona uwezekano wa Kristo kurejelewa kama chemchemi ya uzima kwa sababu yeye ni mto, njia, ambayo kwayo uzima, roho, furaha na mibaraka yote ya Mungu hutiririka ulimwenguni. Roho ya Unabii inasema:

> "Maumbo sawa ya kupendeza na kujieleza yanaonyeshwa katika Bibilia nzima. Karne nyingi kabla ya kuja kwa Kristo, Musa alimwashiria kama Mwamba wa wokovu wa Israeli (Kumbukumbu 32:15); mwandishi wa Zaburi anamuimba kama "mwokozi wangu," "Mwamba wa nguvu zangu," "mwamba nisioweza kuupanda," "mwamba wa makazi yangu," "mwamba wa moyo wangu," "mwamba wangu wa kukimbilia." Katika wimbo wa Daudi neema yake inaonyeshwa kama **"maji matulivu**," **baridi** katikati ya majani mabichi, ambayo Mchungaji wa mbinguni huwaongoza kondoo wake. Tena, "We utawafanya," anasema, "**Nawe utawanywesha mto wa furaha zako. Maana kwako Wewe iko chemchemi ya uzima."** Zaburi 19:14; 62:7; Zaburi 61:2; 71:3 (kiasi); 73:26 (kiasi); 94:22; 23:2; 36:8, 9. Na mtu mwenye hekima anatangaza,

“**Maneno ya kinywa cha mtu ni kama maji ya vilindi; Kijito kibubujikacho; chemchemi ya hekima.” Methali 18:4. Kwa Yeremia, Kristo ni “chemchemi ya maji ya uzima;” kwa Zakaria, “chemchemi iliyofunguliwa ... kwa dhambi na kwa unajisi.**” Yeremia 2:13; Zakaria 13:1. – {PP 413.1}

Isaya anamwelezea kama “mwamba wa milele,” na “kama kivuli cha mwamba mkubwa katika nchi yenye uchovu.” Isaya 26:4 (kiasi); 32:2. Na anarekodi ahadi ya thamani, akiweka wazi kwa mawazo mto uliobubujika kwa Israeli: “Maskini na wahitaji wanatafuta maji, wala hapana; ndimi zao zimekauka kwa kiu; mimi, Bwana, nitawasikia, mimi, Mungu wa Israeli, sitawaacha.” “Kwa maana nitamimina maji juu yake aliye na kiu, na vijito vya maji juu ya mahali pakavu;” “Maana katika nyika maji yatabubujika; na vijito jangwani.” Mwaliko unatolewa, “Haya, kila aonaye kiu, njoni majini.” Isaya 41:17; 44:3; Isaya 35:6; 55:1. Na katika kurasa za mwisho za Neno Takatifu mwaliko huu unarejelewa. Mto wa maji ya uzima, “maangavu kama kioo,” yanatiririka kutoka kwenye kile kiti cha enzi cha Mungu na cha Mwana-Kondoo; na wito wa neema unatolewa kwa vizazi vyote, “na kila anayetaka na anywe maji ya uzima bure.” Ufunuo 22:17. – {PP 413.2}

Katika Zaburi 36, fungu la 8 tunaona kwamba yeyote anywaye kutoka kwa mto huu, hunywa radhi na furaha ya Mungu

Zaburi 36:8 Watashibishwa kwa unono wa nyumba yako, Nawe **utawanywesha mto wa furaha zako**.

Ushirika huu wa kupendeza na Mungu wa furaha na radhi unapitishwa kwetu.

1 Yohana 1:3  Twawatangazia lile tulililoliona na kulisikia ili kwamba nanyi mwe na ushirika nasi na ushirika wetu hasa ni pamoja na Baba na Mwanawe Yesu Kristo.

Kuna nyakati zimeteuliwa kwa burudisho hili. Unatiririka katika Sabato.

Isaya 58:13-14 Kama ukigeuza mguu wako usihalifu **sabato**, usifanye anasa yako siku ya utakatifu wangu; **ukiita sabato siku ya furaha**, na siku takatifu ya Bwana yenye heshima; ukiitukuza, kwa kutokuzifanya

njia zako mwenyewe, wala kuyatafuta yakupendezayo, wala kusema maneno yako mwenyewe; **ndipo utakapojifurahisha katika Bwana**; nami nitakupandisha mahali pa nchi palipoinuka; nitakulisha urithi wa Yakobo baba yako; kwa maana kinywa cha Bwana kimenena hayo.

Pia katika mwezi mpya:

Ezekieli 46:1 Bwana MUNGU asema hivi; Lango la ua wa ndani, lielekealo upande wa mashariki litafungwa siku sita za kazi; lakini siku ya **sabato litafunguliwa, na siku ya mwezi mpya litafunguliwa**.

Ezekieli 46:3 Watu wa nchi nao wataabudu mbele ya mlango wa lile lango mbele za Bwana, **siku za sabato, na siku za mwezi mpya..**

Yesu alitukaribisha tunywe maji ya uzima katika wakati wa sikukuu.

Yohana 7:37-38 Siku ile ya mwisho ya Sikukuu, siku ile kuu, wakati Yesu akiwa amesimama huko, akapaza sauti Yake akasema, Kama mtu ye yote anaona kiu na aje Kwangu anywe. Ye yote aniaminiye Mimi, kama maandiko yasemavyo, vijito vya maji ya uzima vitatiririka ndani mwake.

Kuna uhusiano kati ya mfano wa divai na mto wa uzima kwa sababu divai, kama tu unga na mafuta, hutiririka kupitia kwa maji ya uzima ya mto wa uzima, chemchemi ya uzima, Yesu Kristo, Mwana wa pekee wa Mungu. Katika kusherehekea sikukuu ya vibanda wakati wa Yesu, makuhani wangeadhimisha kuletwa kwa maji kutoka kwa mwamba ulioko Horebu kwa kuleta maji kanisani kutoka Siloamu wakitumia chombo cha dhahabu. Kulikuwa na beseni mbili za fedha, moja ya maji, na nyingine ya divai; hizi mbili zilichanganywa pamoja katika mfereji ulioelekea kwenye bahari. Hili ni sawa kabisa na kile ambacho tunasoma katika Ezekieli 47.

Ezekieli 47:7-8 Basi nikiisha kurudi, tazama, kando ya ukingo wa mto ilikuwapo miti mingi sana, upande huu na upande huu. Ndipo akaniambia, Maji haya yanatoka kwenda pande za nchi ya mashariki, nayo yanashuka mpaka Araba, na kuingia katika bahari maji yatokezwayo yataingia baharini na maji yake yataponyeka.

NIV inaitafsiri hivi:

Ezekieli 47:8 Ndipo akaniambia, Maji haya yanatoka kwenda pande za nchi ya mashariki, nayo yanashuka mpaka Araba, na kuingia katika **bahari** maji yatokezwayo yataingia baharini, na maji yake yataponyeka.

Sikukuu ya vibanda ilikuwa sherehe ya furaha ya mibaraka ambayo Mungu aliwapa Waisraeli. Inawezekana kabisa kuwa mfano wa divai katika sherehe hii pia ulimaanisha furaha. Zingatia kile ambacho Roho ya Unabii inasema:

"Kububujika kwa maji kutoka kwenye mwamba jangwani kulisherehekewa na Waisraeli, baada ya kuishi kwao Kanani, **kwa maonyesho la furaha kuu**. Katika wakati wa Kristo sherehe hizi zilikuwa zimekuwa sherehe za kuvutia zaidi. Ilitendeka katika wakati wa Sikukuu ya Vibanda, wakati watu kutoka sehemu zote za nchi walikusanyika Yerusalemu. Katika kila ya siku saba za Sikukuu makuhani walitoka nje kwa nyimbo na kwaya ya Walawi kuteka maji kwa vyombo vya dhahabu kutoka kwenye chemchemi ya Siloamu. Walifuatwa na umati wa waabudu, wengi kadiri ya uwezo wangekaribia kijito na kunywa kutoka kwake, wakati bidii ya furaha iliinuka, "Basi, kwa furaha mtateka maji katika visima vya wokovu." Isaya 12:3. Kisha maji yaliyotekwa na makuhani yaliletwa hekaluni katikati ya sauti ya tarumbeta na kuimba kwa makini, "Miguu yetu imesimama Ndani ya malango yako, Ee Yerusalemu." Zaburi 122:2. Maji yalimwagwa juu ya madhabahu ya sadaka ya kuteketezwa, nyimbo za kusifu zikiendelea, halaiki ikijiunga kwa viitikio vya ushindi na kwa ala za muziki na tarumbeta zenye sauti-nzito. – {PP 412.1}

**Mkombozi alitumia huduma hii ya mfano kuongoza mawazo ya watu kwa mibaraka ambayo alikuwa amekuja kuwaletea**. **"Katika siku ya mwisho, siku hiyo kuu ya sikukuu," Sauti yake ilisikika katika toni ambazo ziliviringika katika kuta za hekalu, "Kama mtu ye yote anaona kiu na aje Kwangu anywe. Yeyote aniaminiye Mimi, kama maandiko yasemavyo, vijito vya maji ya uzima vitatiririka ndani mwake."** "Haya," anasema Yohana, "aliposema haya alimaanisha Roho Mtakatifu ambaye wote waliomwamini wangempokea." Yohana 7:37-39. Maji ya kunawilisha, yakitoka katika nchi kavu na tupu, yakisababisha jangwa kuchanua, na kububujika kutoa uzima kwa waangamiao, **ni nembo ya neema takatifu ambayo Kristo pekee anaweza kuiifadhi**, na ambayo ni maji ya uzima,

> yatakasayo, kuanawilisha, na kuifanya nafsi. Kwa yule ambayo Kristo anaishi ndani yake ana chemchemi ya neema na uwezo isiyokauka ndani yake. **Yesu hufurahisha maisha na kuangaza njia za wale ambao humtafuta kwa kweli.** Upendo wake, ukipokelewa ndani ya moyo, utabubujika kwa kazi njema hadi kwa uzima wa milele. Na haubariki nafsi tu ambayo unatoka kwayo, bali kijito cha uzima kitabubujika katika maneno na vitendo vya haki, kuburudisha wenye kiu karibu naye." – {PP 412.2}

Mto wa uzima pia ni mfano wa Kristo akimwaga damu yake, uzima wake, ili sisi tuwe na uzima, na mibaraka ambayo Mbingu ilitaka kutupa, ikiwemo furaha ya Baba.

> "Damu ya Yesu hutakasa dhambi zetu zote…. Daima tunahitaji kuweka mbele yetu ufanisi wa damu ya Yesu. **Hiyo damu itakasayo uzima, idumishayo uzima,** ipatikanayo kwa imani ya hai, ndio tumaini letu. Tunahitaji kukua kwa kuthamini thamani yake isiyoweza kupimika, kwa kuwa inanena kwetu tu kama sisi kwa imani tukidai wema wake, kudumisha mawazo safi na kuwa na amani na Mungu. **Hii inawasilishwa kama damu ya kusamehe, kwa muungano usiotenganishwa na ufufuo na uzima wa Mkombozi wetu, ikionyeshwa na kijito kibubujikao daima kutoka kwa kiti cha enzi cha Mungu, maji ya mto wa uzima.** "– {SD 226.2}

> "Mkombozi wetu hakuwa asulubishwa kwa mara ya pili; na ni muhimu tu kwa wale ambao wanatafuta mibaraka ya neema yake kuagiza kwa jina la Yesu, wakiweka wazi mahitaji ya moyo katika maombi kwa Mungu. Ombi kama hilo litaleta mbele za Bwana wa majeshi vidonda vya Yesu, na **kisha itabubujika upya damu itoayo uzima, inayofananishwa na kububujika kwa maji ya uzima kwa Israeli**." – {PP 411.3}

Divai ambayo huwafanya watu kufurahia, hutiririka kupitia kwa mto wa uzima. Kupitia kwa Kristo tunapokea mibaraka yote ilioko, na hili linawezekana kupitia kwa kuchapwa, kukejeliwa, na kupondwa kwa Kristo; Kuteseka kwake na, kumwagika kwa damu yake. Mifano yote ya sadaka hii inazungumzia hili. Ngano lazima ingesiagwa ili kupata unga, mizeituni lazima ingepondwa ili kutoa mafuta, na zabibu lazima zingefinywa au kupondwa ili kutengeneza divai. Kama tukija kwa Kristo anapotuita kwa mibaraka ya

kipekee, tukitambua gharama ambayo yeye na Babake walilipa ili kufanya mibaraka yote iwepo, tutakunywa kwake na kujitumbukiza kwa mto ambao unaongezeka kwa kina baada ya ridhaa 1000 zinazotajwa katika Ezekieli 47[4], na atatutoshelezea kila hitaji, hata hitaji la kukubalika na Baba na kujua kwamba anafurahishwa nasi. Furaha hii itaanzisha msingi wa kujenga mahusiano ya familia imara na yenye afya ambayo pia yataleta furaha maishani mwetu na wakati mwingi wa kufurahia.


> "Kafara moja kubwa ambayo imefanywa ni ya kutosha kwa wale wote watakao amini. Upendo wa Kristo utahuisha waumini na uzima mpya. **Yeyote atakaye kunywa kutoka kwa chemchemi ya uzima, atajazwa na divai mpya ya ufalme.**" 1SM 388.1

Utukufu ni kwa Mungu na Baba ya Bwana wetu Yesu Kristo ambaye hunyesha kwa wanawe mibaraka hiyo mikubwa ya upendo na neema. Utakuja kwa mto huu wa uzima? Utakunywa divai ya ufalme kwanzia Sabato had Sabato na mwezi mpya hadi mwezi mpya? Onja uone kuwa Bwana ni mwema.

---

[4] Inafurahisha zaidi kugundua kwamba katika RVA, SE, RVR na fasiri zingine za Bibilia za Kihispania, Ezekieli 47:9 in basema: "Tena itakuwa, kila kiumbe hai kiogeleacho, kila mahali itakapofika mito hiyo, kitaishi." Njia ya pekee ya kuogelea katika mto na kuishi ni kuendelea kwa mto hadi ridhaa 4000 (tazama Eze. 47:5) ambapo maji yamezidi kichwa na yanaweza vukwa kwa kuogelea. Kama mto unaongezeka kwa kina baada ya ridhaa 1000 (kumaanisha wakati ulioteuliwa) na mibaraka inapanuka na kuongezeka kwa kina nayo, na tunaamua kutoufuata mto hadi mahali ambapo tunaweza ogelea ndani yake, tutakuwa tukipoteza mbaraka mkubwa ambao unahitajika.

Vijitabu vingine vinavyo husiana na mada hii vinapatikana katika maranathamedia.com




**Kusimama kwa vionyeshi**


Harakati ya Wadventista ilijengwa kwa msingi wa Ufunuo 14:12 kama ikiundwa kwa wale ambao wanatunza sheria za Mungu na imani ya Yesu. Kutoka kwa msingi huu, kijitabu hiki kinadhihirisha mwingiliano kwa ufahamu wa haki ya Kristo ambayo inawekwa wazi katika kutii amri zote za Mungu.




**Vipi Kuhusu Sikukuu?**

*Vipi Kuhusu sikukuu?* Kinajibu maswali mengi kama vile:

Sheria inahitaji utunzaji wetu siku ya leo?
Ni nini ambacho kinahusishwa katika sheria?
Je, sikukuu zina kanuni za maadili?
Lazima tutunze sheria ili kuokolewa?




**Kuondoa Miwani ya Agano ya Augustino**

Jifunze jinsi mfumo wa agano uliokuzwa na Augustino ulivyosaidia kukatiza mzunguko wa kupokea mvua ya masika kupitia kwa ujumbe wenye thamani uliohubiriwa katika mwaka wa 1888.

# Mkate Wa Uzima Kutoka Mbinguni

Mfumo wa kutoa sadaka na kafara yake ya wanyama na sadaka ya nyama na vinywaji vyote viliashiria neema ya uzima ya Yesu kupitia kwa huduma yake msalabani na upatanishi wake mbinguni kwa ajili yetu.

Swali linazuka ni nini umuhimu wa uzito na vipimo vya unga na mafuta na viwango vya wanyama? Kama matukio haya yote yaliashiria kifo cha Yesu miaka 2000 iliyopita basi ni jinsi gani kila ya hizi kafara za wanyama na nyama zilitofautiana kwa kila kusanyiko la kidini? Hili linamaana gani?

Kuna mafunzo kwetu katika kafara na sadaka hizi ambayo lazima tuzingatie?

> Sheria ni injili ilivyo, na injili ni sheria iliyofunuliwa. Sheria ni mzizi, injili ni maua ya harufu nzuri na matunda ambayo huzaa. ***Agano la Kale hutoa nuru kuhusu Agano Jipya, na Jipya dhidi ya Kale***. Kila moja ni ufunuo wa utukufu wa Mungu katika Kristo. Kila ukweli wa kisasa ambao utaendelea kudhihirisha ukweli mpya wa ndani kwa kwa mtafutaji asiyechoka. ukweli katika Kristo na kupitia kwa Kristo hauna kipimo. ***Wanafunzi wa maandiko hutafuta, jinsi ilivyo, katika chemchemi ambayo huongezeka kwa kina na upana anavyochungulia kina chake***. Christ’s Object Lessons 128.

Tuweze kujifunza injili zaidi kupitia kwa nuru inayopatikana katika Agano la Kale. Wacha tunywe kutoka kwa chemchemi na tuzidishe kina cha furaha yetu katika injili ya Kristo.